Jumatatu Novemba 23, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580408

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW

**MWALIMU** mbaroni madai ya kujeruhi akigombania pombe

UKURASA 8



**MABALOZI** EU wajadili ukatili wa kijinsia nchini

UKURASA 3



**Solskjaer apagawa ushindi wa kwanza**

UKURASA 20

# Serikali yataja sababu saruji kupanda bei

UKURASA 2



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge, akiangalia moja ya nyumba zilizopo eneo la Kunduchi Mtongani jijini Dar es Salaam, ambazo zipo katika eneo hatari lenye mfumuko wa tope alipotembelea jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

RIPOTI MAALUMU

## Corona ilivyokimbiza wafadhili vituo watoto

UKURASA 4

## Mtaalamu abainisha chanzo mfumuko tope

UKURASA 8

Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

**MICHEZO** **MGUNDA ALIA NA WACHEZAJI KUPIGWA WIKI** UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Serikali yataja sababu saruji kupanda bei

**Na Mwandishi Wetu**



Mtendaji Mkuu na Meneja wa Kiwanda cha Dangote nchini Tanzania, Abdullahi Baba (kushoto), akimwelezea Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Ludovick Nduhiye (wa pili kushoto), matengenezo ya mitambo ya uzalishaji saruji yanavyoendelea alipotembelea kiwanda hicho, kilichopo mkoani Mtwara mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Ludovick Nduhiye, ameeleza sababu ya saruji kupanda bei na kuadimika kuwa ni baadhi ya viwanda kufunga uzalishaji mwezi Oktoba na Novemba, mwaka huu kwa ajili ya ukarabati.

Pia, alisema miradi mikubwa ya kielelezo ambayo huhitaji saruji nyingi ni sababu ya baadhi ya maeneo kuadimika na kupanda bei.

Akizungumza baada ya kufanya ziara ya tathmini kwenye viwanda na mawakala wa saruji kujua hali halisi ya uzalishaji, mwenendo wa bei na usambazaji wa saruji nchini, alisema baadhi ya miradi iliyotajwa kuongeza mahitaji ya saruji ni pamoja na ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Mto Rufiji wa Julius Nyerere Hydropower Project (JNHPP), ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na ujenzi wa daraja la New Selander Dar es Salaam.

Mingine ni mradi wa ujenzi wa barabara za juu Ubungo, mwendokasi awamu ya pili, barabara za mikoani, ujenzi wa viwanja vya ndege, uendelezaji wa makao makuu Dodoma na mahitaji ya watu binafsi ya ujenzi.

Alisema, ziara hiyo ililenga pia kuona jinsi viwanda vilivyojipanga kukabiliana na tatizo hilo la upatikanaji na upandaji holela wa bei ya saruji nchini, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Viwanda vilivyotembelewa ni Twiga na Lake kinachozalisha saruji ya Nyati, vya Dar es Salaam, Dangote cha Mtwara na Mbeya kinachozalisha saruji ya Tembo.

Naibu Katibu Mkuu ambaye alifuatana na maofisa waandamizi toka Wizara ya Viwanda na Biashara, alibaini kuwa kati ya viwanda tisa vinavyozalisha saruji nchini kwa sasa, baadhi yake vilisimamisha au kupunguza kiwango cha uzalishaji mwezi Oktoba na Novemba, kwa ajili ya kufanya matengenezo ya mitambo ya uzalishaji.

Alisema baadhi ya viwanda hivyo vilivyokuwa katika kipindi cha matengenezo yo kawaida ya kila mwaka au kufanya uhuishaji wa mifumo ya uendeshaji na uboreshaji wa miundombinu ya uzalishaji nishati ni pamoja na Dangote, Mbeya na Twiga.

"Baadhi ya viwanda viliendelea na uzalishaji na usambazaji japo kwa kiwango cha chini kidogo.

Kwa sasa viwanda vyote tayari vimekamilisha ukarabati huo na vimejipanga kuongeza uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya soko," alisema.

Awali, Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam, Paulo Mshimo, alisema saruji ilipanda kutoka Sh. 14,500 hadi 19,000, lakini kwa sasa ni kati ya Sh. 14,500 hadi zaidi ya Sh. 15,500.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Kiwanda Twiga, Alfonso Velez, alisema wanaendelea na uzalishaji wa saruji na kuisambaza kwa wateja wake kwa bei ile ile ya Sh. 13,500 kwa mfuko wa saruji aina ya 32.5R na Sh. 13,800 kwa saruji aina ya 42.5R.

Alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha wastani wa tani 160,000 kwa mwezi na takribani tani milioni mbili kwa mwaka na kimejipanga kuongeza uzalishaji.

Wakala wa saruji kutoka Kiwanda cha Twiga, Dipak Manilal Lal, alisema mahitaji ya saruji yameongezeka nchini na huuza yote anayopata kutoka kiwandani, huku akiweka utaratibu wa kila mteja kupata mifuko 100 pekee.

Vile vile, baadhi ya mawakala waliotembelewa jijini Dar es Salaam, walikiri kupokea saruji na kuiuza moja kwa moja kwa wateja wao, tofauti na walipokuwa wakihifadhi inayobaki.

Naye Mkuu wa Idara ya Mikakati ya Kibiashara wa Kiwanda cha Lake, IPN Pathall, alisema uhaba wa saruji nchini ni dalili nzuri ya maendeleo ya kiuchumi unaosababishwa na ongezeko kubwa la mahitaji ya bidhaa hiyo kuliko uzalishaji, linalohimiza viwanda kuongeza uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya soko.

Alisema kiwanda hicho kinachozalisha saruji aina ya Nyati hakikusitisha uzalishaji wala kupandisha bei ikibaki kuwa Sh. 12,710 kwa saruji aina ya 32.5R na Sh. 13,500 kwa saruji aina ya 42.5R.

Mtendaji Mkuu wa uzalishaji Kiwanda cha Lake, Biswajeet Mallik, alisema kiwanda hicho kimeendelea na uzalishaji na tani 50,000 zinazalishwa kwa siku na kwa mwezi 600,000 huku wakijipanga kuongeza uzalishaji.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mtwara, Alphayo Kidata, alisema bei ya saruji ilipanda kutoka Sh. 13,500 hadi Sh. 23,000 na kwamba imeanza kushuka hadi Sh. 14,000 na 15,000 kwa mfuko.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Lindi, Rehema Madenge, alisema kutokana na uhaba wa saruji katika mkoa wake bidhaa hiyo ilipanda hadi kufikia Sh. 24,000 kwa mfuko na sasa imeshuka hadi Sh. 15,000.

Mtendaji Mkuu na Meneja wa Kiwanda cha Dangote nchini, Abdullahi Baba, alisema kiwanda chake kilisimimisha uzalishaji Oktoba 2020 ili kufanya matengenezo ya mitambo yake pamoja na kukamilisha kusimika mitambo ya uzalishaji umeme baada ya kufanya uamuzi wa kimkakati wa kununua mitambo yao wenyewe na kuachana na utaratibu wa kununua nishati hiyo kutoka kampuni nyingine binafsi iliyopewa kandarasi mwaka 2018 ya kuzalisha umeme na kukiuzia kiwanda na kusababisha gharama zaidi.

Akifafanua alisema mchakato wa kuhama kutoka matumizi ya mkandarasi huyo binafsi kwenda utumiaji wa mitambo ya kampuni umechangia kuathiri uzalishaji na upatikanaji wa bidhaa hiyo nchini.

Matengenezo ya mwisho wa mwaka kwa utaratibu wao huwa yanafanywa kila mwaka mwezi Aprili ambao kwa tathmini yao ni mwezi ulio na mahitaji ya saruji kidogo kutokana na mvua nyingi. Hata hivyo, kwa mwaka huu 2020 matengenezo hayo yamefanyika mwezi Oktoba badala ya mwezi Aprili kutokana na ukosefu wa vipuri vinavyoagizwa nje ya nchi kutokupatikana kwa sababu ya janga la corona.

Vile vile, meneja huyo alisema katika kipindi hicho kiwanda kilihuisha mfumo wake wa TEHAMA unaotumiwa katika shughuli zake za utendaji. Zoezi hilo la uhuishaji wa mfumo pamoja na mambo mengine liliathiri usambazaji wa saruji na hivyo kuchangia upatikanaji hafifu usiokidhi mahitaji makubwa ya saruji yaliyoongezeka.

Alisema katika kipindi hicho kiwanda hakikupandisha bei na iliuzwa Sh. 11,860 kwa saruji ya 32.5 na Sh. 12,110 kwa saruji 42.5 bila Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Naye Katibu wa Kampuni na Mshauri wa mambo ya Kisheria wa Kiwanda cha saruji Mbeya, Ian Almachius, alimweleza Naibu Katibu Mkuu kuwa kiwanda hicho kinachozalisha saruji ya Tembo, kilisimamisha uzalishaji kuanzia Oktoba 14 hadi 17, 2020 kwa ajili ya matengenezo ya kila mwaka. Pia, alisema kiwanda hicho kinauwezo wa kuzalisha tani 370,000 kwa mwaka.

Ian alisema mfuko mmoja wa kilo 50 uliuzwa Sh. 13,700 kwa saruji aina ya 32.5 na Sh. 17,200 aina ya 42.5.

Kiwanda hicho kinakabiliwa na tatizo la umeme na uwezo wake mdogo wa kuzalisha 'clinker' ambayo ni malighafi muhimu na wakati huo kushindwa kuipata kwa wakati toka kwenye viwanda vinavyoiuzia.

Serikali imesisitiza kuhusu umuhimu wa kiwanda hicho kupanua uwezo wake wa kuzalisha 'clinker' ili kuendana na uhitaji wa mitambo iliyosimikwa kuzalisha saruji yenye uwezo wa kuzalisha tani milioni 1.1, ili kuongeza ufanisi na tija toka hali ya sasa ya uzalishaji wa asilimia chini ya asilimia 40 ya uwezo uliosimikwa kwa mwaka.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Steven Ndaki, alisema bei ya saruji ilipanda hadi kufikia Sh. 24,000 kwa mfuko na sasa imeanza kushuka na inauzwa kwa Sh. 15,000.

Timu ya wataalamu iliyotembelea, Kiwanda cha Saruji cha Tanga, kinachozalisha saruji kwa jina la Simba, Kiwanda cha Saruji Kilimanjaro, kinachozalisha Kilimanjaro, Kiwanda cha Kimataifa ya Jun Yu inayozalisha saruji aina Moshi, na Kiwanda cha Maweni Limestone kinayozalisha clinker na kuviuzia viwanda vingine vinavyotengeneza saruji.

Viwanda vyote vilivyotembelewa vilikiri kutokupandisha bei ya bidhaa hiyo na kuendelea na uzalishaji na kujipanga kuongeza zaidi ili kukidhi mahitaji ya soko linalokua siku hadi siku.

Tanzania ina viwanda 13 vya saruji, vyote vikifanya kazi ipasavyo vinaweza kukidhi mahitaji yote ya saruji nchini ambayo ni takribani tani milioni sita kwa mwaka na kukidhi mahitaji ya miradi mikubwa inayoendelea nchini.

Viwanda ambavyo vinazalisha saruji kwa sasa ni tisa ambavyo ni Saruji cha Portland Tanzania (Twiga), Kiwanda cha Dangote Group (Dangote Mtwara), Saruji ya Lake ( Nyati), Kiwanda cha Saruji Tanga (Simba), Kiwanda cha Saruji Mbeya (Tembo), Kiwanda cha Saruji Kilimanjaro (Kilimanjaro). Viwanda vingine ni cha Saruji cha Fortune (Diamond), Kampuni ya Amsons (Camel) na Maweni Limestone inayozalisha clinker.

Viwanda ambavyo vilikuwa vinazalisha saruji na kwa sasa vimesimamisha uzalishaji kutokana na sababu mbalimbali ni pamoja na Xinghao Group (Lulu), Kampuni ya Saruji Kisarawe (lucky), Kampuni ya Saruji Arusha na Kampuni ya Uchimbaji ya Athi River (Rhino).

## HABARI KITAIFA

# Jela miaka 30, viboko 12 kwa kubaka mtoto

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imemhukumu mkazi wa Kijiji cha Nyeunge, Lugwisha Makungu (20), kutumikia kifungo cha miaka 30 jela na viboko 12 kwa kosa la kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka 16.

Mtoto huyo (jina linahifadhiwa), ni mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Nyawilimilwa.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samueli Maweda, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Clemence Kato, alipeleka mashahidi wanne na vielelezo vitatu, ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Hakimu Maweda alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa vijana wengine wenye tabia ya kubaka kama yake.

Alisema siku ya tukio hilo mwanafunzi huyo alikuwa amelala na mdogo wake kwenye nyumba na wazazi wake, walikuwa wamelala nyumba nyingine ilipofika majira ya saa tatu usiku, mshtakiwa huyo alifika alipokuwa amelala mwanafunzi huyo na kumrubuni kuwa anataka amuoe.

Alisema mshtakiwa huyo baada ya kumrubuni mwanafunzi huyo alimchukuwa katika Kitongoji cha Ntinachi majira ya saa tatu usiku na kumpeleka kwao katika Kijiji cha Nyeunge kwa madai kuwa atamuoa.

Alisema baada ya mshtakiwa na mwanafunzi huyo kuondoka, mdogo wake alibaki amelala na asubuhi yake, baba yake mwanafunzi huyo alimuuliza mdogo wake alipo dada yake, alijibu kuwa mshtakiwa alimchukua usiku na kuondoka naye.

Awali akisoma hati ya Mashtaka Wakili wa Kato alidai Juni 23, mwaka huu majira ya saa tatu usiku katika Kijiji cha Nyawilimilwa Kitongoji cha Ntinachi mkoa wa Geita mshtakiwa alimbaka binti huyo.

# Mabalozi EU wazungumzia ukatili wa kijinsia nchini

**Na Salome Kitomari**

MABALOZI watano wa Umoja wa Ulaya (EU) nchini, wamesema jitihada zinahitajika kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake, ambayo ni kikwazo cha ukombozi na maendeleo ya wanawake.

Wakizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano na waandishi wa habari, mabalozi hao wa Ufaransa, Ujerumani, Ubelgiji, Uholanzi, Mkuu wa Umoja wa Ulaya nchini, Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa unaoshughulika na Wanawake (UN Women), walisema katika maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili watashiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Mkuu wa EU nchini, Manfredo Fantl, alisema katika kuadhimisha siku 16, EU itaendesha shughuli za kijamii kwa ajili ya kuelimisha na kuhamasisha jamii kuvunja mnyororo wa ukatili dhidi ya wanawake kwa kuwawezesha kiuchumi katika sekta isiyo rasmi.

"Katika kuadhimisha siku hii EU na wanachama wake kutakuwa na matukio ya kijamii ambayo yatabeba ujumbe wa maendeleo ya mwanamke ni faida kwa jamii nzima na kauli mbiu ya Tanzania ya tupinge ukatili wa kijinsia. Mabadiliko yanaanza na mimi," alisema. Fantl alisema matukio hayo yatahusisha pia wanaume ambao ni sehemu ya suluhisho, na kwamba bado hakuna usawa katika ajira, mishahara na uangalizi licha ya wanawake kuingia katika nafasi mbalimbali.

"Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Ofisi Kuu ya Takwimu Tanzania (NBS), wanawake ni asilimia 51 ya nguvu kazi katika sekta isiyo rasmi, sekta binafsi inatawaliwa na wanaume zaidi ambao ni asilimia 72 ya wajasiriamali huku wanawake wakiwa ni asilimia 28," alisema.

Alisema pia kuna ukandamizaji wa wanawake katika ajira na ajira binafsi, huku asilimia 81 ya wanaume wanalipwa zaidi ya Sh. milioni 1.5, huku wanawake asilimia 15 wanapata kipato hicho wakiwa sekta binafsi.

Balozi wa Ufaransa Frederic Clavier, alisema miaka 10 iliyopita UN Women ilianzishwa baada ya uragibishi uliofanywa na nchi yake, na kwamba wataendelea kufanya kazi kwa pamoja kutekeleza miradi inayogusa na kubadilisha maisha ya wanawake.

Alisema Ufaransa inataka kuwa mfano katika usawa wa kujinsia kwa kuongeza idadi ya wanawake katika nafasi za meneja na mabalozi na kwamba asilimia 26 ya mabalozi ni wanawake, huku kuweka katika mpango kazi wa wizara na mashirika 12 ikiwamo Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD). Alisema pia wameongeza fedha maalum za kusaidia mashirika yasiyo ya kiserikali kwa miaka mitano ijayo kwa Euro milioni 120 kwa miradi mbalimbali, na kwa Tanzania watafadhili miradi miwili ya kuwajengea uwezo wanawake wa shughuli za kilimo ambao wanachangia asilimia 50 ya chakula na robo tatu ya nguvu kazi huku wakipata asilimia 10 ya kipato.

Alisema Ufaransa itatoa Euro milioni 1.5 kwa miaka miwili ijayo kwa ajili ya kuwajengea uwezo wanawake na kipaumbele kikiwa ni kupinga ukatili dhidi ya kundi hilo.

Katika kuadhimisha siku 16 Ufaransa, Ubelgiji na mashirika mengine atakuwa na mdahalo katika taasisi za elimu kuhusu unyanyasaji kingono, wanawake katika nafasi za maamuzi na ndoa za utotoni, na baadaye kwa kushirikiana na wajumbe wa EU atakuwa na usiku wa burudani ukiwa na kauli mbiu ya 'usiku wa kuwawezesha wanawake'.

Naye Balozi wa Ujerumani, Regine Hess, alisema wamekuwa mstari wa mbele kusaidia masuala ya jinsia kwa kufadhili miradi mbalimbali kama vyoo kwa wasichana 500 na mahali pa kubadilishia pedi katika shule ya msingi na sekondari mkoani Iringa.

Pia, wametoa semina na hamasa kwa wasichana wadogo 3,500 kwa masuala ya unyanyasaji kingono, magonjwa yanayoambukiza na ukatili wa kijinsia wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, utengenzaji wa pedi kwa wasichana zaidi ya 3,000 mkoani Pwani na filamu inayoelimisha jinsi msichana anaweza kujikinga na ukatili wa kingono na ukatili wa kijinsia.

Naye Balozi wa Uholanzi, Lianne Houben, alisema wanafadhili miradi ya kupinga ukatili wa kijinsia kama Children Diginity Forum kupinga ukeketaji, ndoa za utotoni Mpwapwa mkoani Dodoma na kata ya Kitunda jijini Dar es Salam.

Pia, matamasha ya sauti za busara ambayo ina kauli mbiu ya kupinga unyanyasaji kingono, na kwamba wataendelea kusaidia miradi hiyo na watazindua filamu ya ukatili wa ngono.




Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akikabidhiwa mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 100 na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kulia), ikiwa ni mchango wa mbio za NBC Marathon zilizofanyika jijini Dodoma jana, katika kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya kizazi nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgogoro wa ukusanyaji wa mapato mgodini watatuliwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI imetatua mgogoro wa usimamizi na ukusanyaji wa kodi za serikali katika mgodi mdogo wa Mwime Two Gold Rush katika Kata ya Zongomela Halmashauri ya Kahama Mjini mkoani Shinyanga.

Suluhu ya mgogoro huo imefikiwa baada ya kupatikana kwa kikundi cha Isalenge Gold Rush kilichoshinda zabuni ya ukusanyaji wa kodi za serikali.

Mgogoro huo uliodumu kwa wiki tatu, ulihusisha vikundi viwili vya Mwime Two Gold Rush na Isalenge Gold Rush ambapo na kila mmoja alitaka kusimamia na kukusanya kodi za serikali, hivyo kusababisha mvutano kabla ya serikali kuingilia kati na kutoa uamuzi.

Pia mgogoro huo ulisababisha Baraza la Ardhi la wilayani hapa kuzuia shughuli za uchimbaji wa madini katika eneo hilo, wakati kisheria baraza halikuwa na mamlaka ya kuingilia masuala ya uchimbaji madini.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Prof. Saimon Msanjila, ndiye aliyeutatua mvutano huo juzi wakati akizungumza na wachimbaji wadogo wa eneo hilo, na kuwataka kutoendeleza migogoro isiyokuwa na tija badala yake wajikite katika shughuli za uchimbaji wa dhahabu ili kujikwamua kiuchumi.

Alisema kikundi cha Isalenge Gold Rush ndicho kilichoshinda zabuni ya kuusimamia mgodi huo kwa niaba ya Tume ya Madini, ili kuhakikisha serikali inapata mapato kupitia kodi zinavyotozwa, hivyo mmmni vyema wakazingatia na kuheshimu uamuzi uliotolewa.

"Vikundi hivi vimekuwa zikilumbana juu ya usimamizi na umiliki wa eneo hili, mchakato wa kumpata msimamizi huyu umezingatia maelekezo na miongozo inayotolewa na serikali kuhusu namna bora ya usimamizi wa shughuli za madini, hivyo atasimamia na kukusanya kodi," alisema Prof. Msanjila.

**RIPOTI MAALUM:**

# Corona ilivyokimbiza wafadhili vituo vya kulelea watoto yatima-1

Na Elizabeth Zaya

NI miezi kadhaa ya 'Tanzania bila corona.' Lakini kwa sekta mtambuka, kila mmoja analia na athari zake, ama kwa wakati huo au mambo kutorejea katika hali yake ya kawaida.

Nipashe imeanzisha safari mahsusi katika eneo ambalo huenda halirushiwi jicho na wengi, lakini ni muhimu katika jamii ambalo ni la vituo vya kulea watoto yatima. Safari hii ilianzia katika kituo cha kulelea yatima cha Mwandaliwa, Mbweni, wilayani Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Haji Bakhulla, anaeleza kilichokisibu kituo chake chenye watoto 76, kutokana na ugonjwa wa corona.

Licha ya kujigamba kufanikiwa kuvuka wimbi la msukosuko huo, anasema bado mambo hayajakaa sawa kama ilivyokuwa awali.

"Nikwambie tu ukweli, kama tunavyosikia sekta nyingine kuyumba kutokana na uwapo wa ugonjwa huu, ndivyo ilivyo na hapa kwetu, kiukweli, hali ni mbaya sana...

"Kabla ya hapa kwetu Tanzania kuingia ugonjwa huu, sisi tulikuwa tumeshaanza kupata athari, kwa sababu baadhi ya wahisani kutoka nchi za nje wanaotusaidia walikuwa wameshakumbwa na ugonjwa huu na walisitisha misaada mapema sana.

"Hali hii ilianza kuwa mbaya hasa kuanzia Desemba 2019, kwa mfano asilimia kubwa ya misaada ya chakula, nguo za watoto na vifaa vyao vingi vya shuleni vilikuwa vinatoka kwa wahisani kutoka nje.

"Wao walikuwa wakija hawatupatii fedha, isipokuwa walikuwa wananunua moja kwa moja vyakula vyote wanaleta. Kwa hiyo, walipozuiwa kuja kwa sababu ya corona, vitu vyote hivyo vilisitishwa na ndipo kuhangaika kulipoanza.

**NGUO ZAADIMIKA**

Bakhulla anasema, nguo kwa watoto ziliisha na kujikuta wanavaa nguo zilizopauka kwa sababu zote walikuwa wanaletewa na wahisani kutoka nje.

"Kama unavyojua watoto kama wakizoeshwa maisha fulani halafu ghafla yanakatishwa, huwa ni vigumu sana kuelewa maana wengi ni wadogo na uelewa wao ni mdogo."

**MAISHA MAGUMU**

Anasema walipojaribu kuwasiliana na wahisani wao hawakufanikiwa kwa sababu utaratibu wao wa kuwasaidia haukuwa wa kuwapatia fedha bali ulikuwa wa kuwasaidia mahitaji kama chakula na mavazi.

Pia, baadhi ya wahisani walikuwa wanawaambia hawawezi kuwasaidia kwa sababu hata wao hali yao ni ngumu.



Baadhi ya watoto wanaolelewa katika kituo cha yatima cha Bunju A. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

Mkurugenzi huyo anasema, baada ya kuelemewa na ugumu wa kuwalea watoto hao, walianza kuwasiliana tena na wahisani wao kwa kuwapigia simu, kuwaandikia barua pepe, kuomba mwendelezo wa hisani zao kutokana na hali ngumu ya maisha.

"Wengine walitujibu na wao hali yao ni ngumu hivyo tuendelee kuvumilia mpaka hali ya kiuchumi itakapotengamaa watatusaidia," anasema Bakhulla.

"...wengine walijibu hawawezi kutusaidia mpaka baada ya mipaka kufunguliwa."

**NAULI YAWA KIKWAZO**

Bakhulla anasema, hali ilizidi kuwa mbaya na kushindwa kutoa nauli kwa wanafunzi wote baada ya likizo ya corona isipokuwa kwa wadogo zaidi wasioweza kutembea wenyewe.

"Ilifikia wakati tukawa tunalazimika kuwaambia watoto wetu hasa wale ambao tunaona wanajielewa, kuanzia darasa la nne mpaka darasa la saba watembee kwenda na kurudi shuleni."

"Tulifanya hivyo ili kile kiasi kidogo cha fedha kilichopo tuwapatie wadogo zao wa darasa la kwanza hadi la tatu ambao tunaona ni wadogo sana ili wapande daladala kwenda shuleni kuliko kutembea kwa sababu ni hatari kwao kutokana na umri wao," anasema Bakhulla.

"Uzuri ni kwamba wengi wa watoto wetu wanasoma katika shule ambazo haziko mbali sana, hawezi kutumia zaidi ya nusu saa au dakika 20 kutembea, akiamka mapema anawahi na hachoki sana."

Anafafanua kwamba, sehemu kubwa ya watoto katika kituo hicho wanasoma katika shule za msingi zilizopo maeneo ya Boko, Mbweni mwisho, Mabwepande, Basihaya, Bunju A na Bunju B, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni.

**PIGO JINGINE**

Baada ya kupata pigo kutoka kwa wahisani nje ya nchi, walipata jingine kutoka kwa wazawa wachache ambao walikuwa wakiwasaidia.

Bakhulla anasema, ilikuwa heri kwao angalau neema kutembelewa na wahisani wazawa, kwa sababu walikuwa na uwezo wa kuwaachia chochote, lakini bahati mbaya nao walikata mguu na hivyo kujikuta wamekosa kote.

"Makundi mbalimbali huwa yanakuja kututembelea na kutuletea vitu mbalimbali ikiwamo pesa taslimu, vyakula na mavazi japokuwa sio kwa kiwango kikubwa kama ilivyo kwa wahisani wa nje.

"Lakini, ujio wao ulikuwa unasaidia sana. Hali ilikuwa mbaya zaidi kwa sababu hata hawa wa ndani walikata mguu na kutufanya tusiwe na mahali popote pa kuegemea."

"Hapa ndipo nilichanganyikiwa kabisa, mimi siku zote huwa namtumaini Mwenyezi Mungu...hapa ndipo nilikazana sana kumuomba ili afanye mbinu kuwasaidia watoto wake wasife njaa, nilikuwa siamiani kinachokwenda kutokea," anasema Bakhulla.

**WAGEUKA OMBAOMBA**

Hali ilizidi kuwa mbaya siku hadi siku na kulazimika kuanza kuangalia orodha ya wadau wao wote wanaowafahamu, ambao walikuwa wakiwatembelea kituoni hapo wa ndani na nje ya nchi.

"Tulifikia kipindi ambacho tukifanikiwa kupata chakula cha leo, tunashukuru Mungu, wakati huo huo, hatujui kesho itakuwaje, tunakuwa hatuna uhakika."

"Tulichokuwa tunakifanya ni kupiga simu kwa mtu mmoja baada ya mwingine, kuomba msaada angalau tupate chakula cha siku cha watoto."

"Lakini, bado ilikuwa tabu sana kupata, tulikuwa tunashangaa hata kwa wale ambao walikuwa wanatusaidia kwa kiwango kikubwa walisema wana hali mbaya. Kila mtu ukimpigia anakujibu hivyo, kwa kipindi kile unaweza kujikuta unamchukia mtu bila sababu kwa kuwa amekataa kukusaidia."

**MIUJIZA**

Walilazimika kuzidisha maombi kwa Mwenyezi Mungu ili awape nguvu na kuwavusha katika hali hiyo ngumu.

"Ilifika wakati hata yule mtu mmoja mmoja aliyekuwa anatupigia simu kutujulia hali na kutupatia chochote kitu nao walikata. Mimi siku zote huwa ni mtu wa kumtegemea Mwenyezi Mungu, ilibidi nizidishe maombi maana hali haikuwa ya kawaida na ukiwaangalia wale watoto ndiyo unachanganyikiwa."

"Kupiga simu na kuomba yalibaki ni maisha yetu ya kila siku, ilibidi unapiga simu na kuomba mtu akusaidie chochote hata kama ni kidogo alichonacho, kama ana mkaa, unga hata kidogo ili mradi watoto wasilale na njaa, kwa kufanya hivyo wengine walikuwa wanasikia huruma wanatupatia hata kidogo chochote."

**KITUO CHA HOPE WALIA SHIDA**

Kituo cha kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu, Hope, chenye watoto 105, Boko, jijini Dar es Salaam, pia kimelalamika kuathiriwa kwa kiwango kikubwa na mlipuko wa ugonjwa wa corona, ulishababisha wahisani kusitisha misaada.

Katibu Mtendaji wa kituo hicho, Hamad Kondo, anasema asilimia kubwa ya wafadhili wao ni wahisani kutoka nje ya nchi na walianza kuathirika mwezi Aprili, mwaka huu.

Anasema kituo hicho kilikuwa kinasaidiwa na wahisani kutoka nchi ya Kuwait kwa upande wa elimu, Saudi Arabia, katika afya na Uturuki upande wa chakula.

Anasema pamoja na akiba kubwa ya chakula ambayo iliwasaidia kutumia katika miezi kadhaa baada ya wahisani kusitisha misaada yao, ilipofika Aprili mwaka huu, kiliwaishia na hali kuanza kuwa mbaya.

Hata hivyo, anasema katika eneo la afya hawakuathirika sana kwa sababu tayari watoto walikuwa wamekatiwa bima ya afya, wala mavazi isipokuwa upande wa chakula.

**RATIBA YA CHAKULA**

Anasema ratiba ya chakula waliyokuwa wanaitumia kabla ya ugonjwa wa corona waliipangua na kuanza kupika kulingana na kinachopatikana.

Kabla ya athari za ugonjwa huo, kwa siku walikuwa wakipika mchele kilo 15 kwa mlo mmoja na hupikwa kwa wiki mara tatu, lakini baada ya ugonjwa walipunguza siku za kupika mchele na kipimo kilipungua hadi kilo 10.

"Katika kuwapakulia tumepunguza kipimo ili kiwatoshe wote, mwanzoni kabisa wakati tumeanza kufanya hivyo, watoto walikuwa wanalia sana wanalalamika kwamba hawashibi, lakini tukawa hatuna jinsi na tunaona wanazoea kidogo kidogo," anasema Kondo.

**WAGOMA KULA MAKANDE**

Kondo anasema hataisahau siku ambayo walikosa chakula kingine na kulazimika kupika makande.

"Kuna siku tuliwapikia makande, tulikuwa hatuna chakula kingine, watoto walikataa kabisa kula pamoja na kuwalazimisha, hii ndiyo siku ambayo tulipata wakati mgumu zaidi."

Kabla ya corona walikuwa wanapika nyama mara tatu kwa wiki, lakini kwa sasa wanapika mara moja na siku zote hupika mboga za majani, maharagwe na kabichi.

Kondo anasema kawaida katika kituo chao huwa na akiba ya chakuka cha zaidi ya miezi mitatu, lakini kwa sasa hakuna.

"Kiukweli hali ya maisha katika vituo vyetu vya kulelea watoto ni ngumu sana, sisi wote tunaofanya huduma hii tunajuana, imefika mahali tuwe tunasaidiana, hapa kwetu tunaona pana unafuu, kuna baadhi ya wenzetu wana hali ngumu zaidi na huwa tunasaidiana pale panapowezekana," anaeleza Kondo.

●**Usikose sehemu ya pili ya ripoti hii kesho.**

# Tanzania yaweka mikoa 20 kimkakati kilimo korosho

**Na Ashton Balaigwa,**
SINGIDA

TANZANIA imeweka mkakati wa kuliteka soko la korosho duniani kwa kuanza kupanua kilimo hicho kutoka mikoa mitano inayolima sasa hadi 20 kutokana na kuwapo kwa mahitaji makubwa ya bidhaa hiyo.

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), imeanza kuwanoa wakulima wa mikoa mbalimbali wakiwamo wa Singida kupitia zao hilo linaloonekana kuwa bora kama ilivyo kwa mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara.

Kutokana na mkakati huo TARI kupitia kituo chake cha Naliendele mkoani Mtwara, kimezalisha aina 54 za mbegu bora za korosho za teknolojia ya kisasa na kuwapatia wakulima wa Wilaya ya Manyoni ambao wameanza kilimo cha pamoja (Block Farming), chenye jumla ya ekari 22,000 katika kijiji cha Masigati wilayani humo.

Akitoa taarifa kwa Bodi ya Wakurugenzi wa TARI iliyotembelea shamba hilo, Kijiji cha Masigati wilayani Manyoni, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema mpango huo ni utekelezaji wa agizo la Rais Dk. John Magufuli la kuongeza uzalishaji na tija wa mazao ya kimkakati ikiwamo korosho.

Alisema kuwa TARI imeanza kutekeleza maono serikali ya kuongeza uzalishaji wa zao hilo kwa vitendo kutoka tani 300,000 za sasa hadi milioni moja ifikapo 2024 na ili kufanikisha wanatekeleza kwa kutumia mbinu bora za kilimo, matumizi ya mbegu bora na viutilifu katika mikoa hiyo mipya ikiwamo wa Singida.

"Tunataka kumtoa mkulima kutoka hali ya chini kabisa ili awe bilionea kupitia mazao ya kimkakati kupitia kilimo na korosho ndio itawatoa wakulima wa mkoa wa Singida kwa kuwa inaonyesha inastawi vizuri ikilinganishwa na mazao mengine, ndio maana TARI imeamua kuweka nguvu ya kutosha katika mkoa huu," alisema.

Alisema TARI inataka kumtoa mkulima kutoka kilimo cha kujikimu na kufanya cha kibiashara ili aweze kuwekeza na kunufaika kupitia kilimo hicho na kuchangia uchumi wa mkulima mmoja mmoja pamoja na uchumi wa taifa kupitia zao hilo la korosho.

Mwenyekiti wa Bodi ya TARI, Dk Yohana Budeba, alisema Bodi hiyo imejipanga kuhakikisha maagizo ya Rais Dk. John Magufuli, yanatekelezwa kwa wakati ikiwamo ya kupanua zao la korosho kutoka mikoa mitano iliyokuwa ikilimwa na kufikia 20 na utekelezaji umeshaanza kwenye mikoa hiyo mipya. Alisema mwanzoni korosho ilikuwa ikilimwa katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma,Tanga na Pwani, lakini kupitia bodi ya TARI sasaivi wameshafika mikoa 20 ya hapa nchini lengo lake ni kuongeza malighafi zinazohitajika katika Viwanda hapa nchini asilimia 60 itoke kwenye kilimo.

"Bodi ya TARI itahakikisha inasimamia ili mipango yote ya serikali pamoja na maagizo yake yote yanafikiwa ikiwamo ya kuzalisha ajira kwenye viwanda kwa kupitia malighafi za kilimo ili kuinua uchumi wa nchi," alisema Mwenyekiti huyo wa bodi.

Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Rahabu Mwagisa, alisema waliamua kuja na mkakati wa kilimo cha korosho kama zao mbadala la biashara kama mengine ya ufuta na dengu ili kuinuka kiuchumi baada ya watafiti kutoka TARI kuwahakikishia zao hilo kustawi kwa wingi katika mkoa huo. Alisema kwa kuanzia walimua kufungua shamba lenye ukubwa wa ekari 22,000 kwaajili ya kufanya kilimo cha pamoja na kuagiza mbegu bora za korosho kutoka TARI Naliendele pamoja na kupatiwa wataalam wa kutoa elimu ya zao hilo. Naye Mkurugenzi wa TARI Naliendele, mkoani Mtwara, Dk. Fortunatus Kapinga, alisema Mkoa wa Singida ni miongoni mwa itakayofanya vizuri kwenye uzalishaji wa korosho na Tanzania kuliteka soko la dunia.




Mchora katuni wa Gazeti la Nipashe, Abdul Kingo, akionyesha cheti cha ushiriki wa mafunzo ya usalama barabarani katika maonyesho ya katuni za kuwakumbuka waathirika wa ajali za barabarani, yaliyofanyika katika kituo cha mabasi ya mikoani Ubungo. Aliyekabidhi cheti ni Kamanda wa Kikosi cha Polisi cha Usalama Barabarani, Mkadam Mkadam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wakazi Mwanza watakiwa kuhama kwenye mafuriko

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

KAMATI ya maafa ya Wilaya ya Nyamagana jijini Mwanza, imewashauri wakazi wa kata za Mabatini, Mbugani na Mirongo kuhamisha makazi yao kandokando ya Mto Mirongo, kutokana na mafuriko ya maji kutoka katika mto huo yaliyosababisha nyumba 22 kubomoka na kuanguka.

Ushauri huo ulitolewa jana na mratibu wa kamati hiyo, Masatu Magafu, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu madhara makubwa ya mafuriko yaliyotokea kwa wakazi wa kata hizo.

"Mafuriko ya maji yaliyotokea Novemba 18 jijini hapo, yaliwashangaza wengi, kwa sababu mvua iliyonyesha hapa mjini ilikuwa ni manyunyu, mvua iliyoleta mafuriko kupitia Mto Mirongo ilinyesha nje ya jiji letu, hivyo nawashauri wakazi hao kuhama kwenye kingo za mto huo, na kutafuta maeneo salama ya kuishi," alisema.

Magafu alisema nyumba 15 zilibomoka na kuanguka katika Kata ya Mabatini na nyumba saba katika Kata ya Mbugani.

Katika Kata ya Mirongo, mali na bidhaa mbalimbali ziliharibiwa na zingine kusombwa na maji, ikiwamo daraja kuvunjika na kivuko chake katika mitaa ya Majengo Mapya na Nyerere 'A', hali iliyosababisha wananchi kukosa mawasiliano.

Alisema baadhi ya mali zilizoharibiwa ni meza 33, bidhaa mbalimbali za wajasiriamali vikiwamo vifaa vya umeme, saa za ukutani, mkononi, nguo na kwamba ushauri huo utaondoa malalamiko ya wananchi kuitupia lawama serikali kuwa haiwasaidii wanapokumbwa na vikwazo hivyo.

Kuhusu matengenezo ya daraja hilo, alisema Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) ndio yenye jukumu la kuhakikisha huduma hiyo inarejea.

# Mradi wa SWIOFish waongeza idadi ya samaki wanaovuliwa

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, kupitia mradi wake wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish), umesaidia kuongezeka kwa samaki wanaovuliwa.

Akifungua kikao cha wataalamu wa sekta hiyo na wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo (Sekta ya Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah, alisema mradi huo umesaidia kuwezesha utafiti mbalimbali na matokeo yake kutumika kurekebisha baadhi ya kanuni za uvuvi.

Alisema umesaidia pia kuongeza uvuvi wa karibu na wa kutumia ndoano kwa maeneo mengi.

"Mfano marekebisho ya kanuni ya uvuvi ya mwaka 2009 kuhusu kubadilisha ukubwa wa macho ya nyavu za kuvulia dagaa kuwa milimita nane badala ya 10 na kumeongeza tija kwa wavuvi wa dagaa ameneo ya Pwani," alisema Dk.Tamatamah.

"Vilevile, baadhi ya samaki waliokuwa wametoweka wameanza kuonekana ikiwamo samaki aina ya sangoro na wengine, na haya ni matokeo ya kuimarisha kwa usimamizi wa rasilimali za uvuvi nchini."

Dk. Tamatamah alisema mradi wa SWIOFish umefadhili pia mafunzo ya uvuvi endelevu ambayo yamesaidia kuongezeka kwa uelewa kwa jamii ya Pwani na kwamba elimu hiyo imechangia baadhi ya wavuvi kutekeleza kwa hiari usimamizi za bahari.

"Jamii ya wavuvi wa Songoro wilayani Kilwa na Ushongo wilayani Pangani, wameamua kufunga shughuli za uvuvi wa Pweza na kuvua kwa kipindi maalum kila baada ya miezi mitatu kwa ajili ya kuruhusu samaki hao kukua ili kuvuliwa katika kiwango kinachoruhusiwa kisheria," alisema Dk. Tamatamah.

"Uanzishwaji wa vikundi 50 vya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi katika wilaya tano za mfano umewezeshwa na mradi huu na kuimarisha utunzaji wa mazingira ya Pwani ambako ukataji wa misitu ya mikoko umepungua na imekuwa ikipandwa katika vijiji mbalimbali kwa lengo la kutunza mazingira."

Dk. Tamatamah alisema usafi wa fukwe katika maeneo ya mradi umeboreshwa na kwamba uchimbaji wa mchanga katika fukwe hususani Bagamoyo mkoani Pwani umepungua kwa kiasi kikubwa.

"Mafanikio mengine ambayo yametokana na SWIOFish ni pamoja na mapato yatokanayo na uvuvi hususani kwenye halmashauri ambako mradi unatekelezwa," alisema Dk. Tamatamah.

Alisema kwa Halmashauri ya Pangani mapato hayo yameongezeka kutoka Sh. milioni 55 mwaka 2016/17 hadi kufikia Sh. milioni 235 mwaka 2018/19.

Kadhalika, alisema mradi huo wa miaka sita ulioanza kutekelezwa mwaka 2015 umedhibiti kwa asilimia 100 za uvuvi haramu wa kutumia baruti na mabomu, hatua ambayo imetokana na kuimarishwa kwa doria pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa jamii ya Pwani kuhusu madhara ya uvuvi haramu.

Mradi huyo unatekelezwa maeneo ya Pwani ya Tanzania katika wilaya za mfano za Mkinga, Jiji la Tanga, Pangani, Bagamoyo, Lindi Vijijini na Chalinze.

Memeja wa mradi huo, Dk. Nicholous Mlalila, alisema pamoja na mambo mengine yanayotekelezwa, wanakusudia kulikarabati Soko la Feri jijini Dar es Salaam kutokana na miundombinu yake kutokuwa rafiki.

Alisema soko hilo lilipojengwa, eneo lilikuwa la kuhudumia watu kati ya 1,500 hadi 3,000 lakini sasa kuna watu 12,000.

Kaimu Mkurugenzi wa Uvuvi, Ezra Byarugaba, alisisitiza umuhimu wa elimu kwa jamii ili ifahamu kuwa rasilimali za uvuvi ni za kwao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# FCC isaidie mchakato mabadiliko Simba SC

**WANACHAMA** na mashabiki wa Simba na Watanzania kwa ujumla wanatamani kuona mchakato wa mabadiliko Simba unakamilika na klabu hiyo kuendeshwa kwa mfumo mpya wa hisa, ambao utasaidia kukua kwa soka si la klabu pekee, bali la Tanzania kwa ujumla.

Hata hivyo, baada ya siku chache zilizopita Mwenyekiti ya Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Mohammed "Mo" Dewji, kueleza mchakato wa mabadiliko ya uendeshaji wa klabu hiyo bado upo mikononi mwa Tume ya Ushindani (FCC), wiki iliyopita tume hiyo iliibuka na kufafanua mambo kadhaa pamoja na kukanusha kuwa wao si kikwazo cha kuchelewa kwa mabadiliko hayo.

Katika taarifa hiyo, FCC ilieleza kufanya uchambuzi wa awali wa maombi ya Simba Sports Club Company Limited ya kupatiwa mwongozo wa kisheria chini ya Sheria ya Ushindani kuhusu namna ya kushughulikia mchakato wa mabadiliko unaohusisha Kampuni za Simba Sports Club Holding Company Limited, Mo Simba Company Limited, Simba Sports Club Company Limited na Klabu ya Simba.

Na baada ya hapo, FCC ilieleza kufanya vikao viwili kati yake na Simba Sports Club Company Limited hadi Julai 24, 2020 na wadaawa (wapeleka maombi) kuelewa mwongozo wa kisheria na kuahidi kuutekeleza kama walivyoelekezwa.

Yapo mambo mengi ya msingi FCC, imeyafafanua ambayo wadaawa walipaswa kuyatekeleza, lakini ikumbukwe mfumo huu wa mabadiliko ya uendeshaji wa klabu ndiyo kwanza unaingia katika soka letu na Afrika Mashariki kwa ujumla, hivyo ni mchakato unaohitaji ushirikiano wa kila upande ili kuuwezesha kwa faida ya soka letu. Kama ambavyo, Simba ilianza awali kwa kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT), ambacho ni chombo kingine cha serikali, tunatambua yapo maelekezo mengi ambayo ilipewa ikitakiwa kuyatekeleza wakati huu ikiendelea na mchakato huo. Hata hivyo, kinachoonekana kwa sasa ni kuwapo kwa baadhi ya taratibu ambazo pengine wadaawa walitekeleza kulingana na maelekezo kutoka BMT wakati huo huo, kwa FCC kwao yakionekana kama ni ukiukwaji wa sheria kabla ya hatua ambayo mchakato huo umefikia.


Mfano ni hatua ya FCC kutaka ufafanuzi kuhusu uteuzi wa Mtendaji Mkuu (CEO) wa Klabu ya Simba kabla ya uwekezaji kufanyika, suala ambalo kwa upande wa wadaawa wametumia mabadiliko ya katiba yao ikiwamo maelekezo ya BMT kwa kuwa na kipindi cha mpito kwani klabu inaendelee kushiriki kalenda mbalimbali za ligi na haisimami ili kusubiri mchakato huo kukamilika.Si lengo la Nipashe kusimama upande wowote katika mkanganyiko huu, kwani kwa namna tulivyofuatilia hatua kwa hatua, tunaamini tofauti ama utata unaojitokeza katika kukamilika kwa mchakato huo, zinatokana na mwingiliano wa kanuni zinachongiwa na ugeni wa suala la mabadiliko kwa klabu ambayo ilikuwa ikiendeshwa na wanachama.

Hivyo, kuna haja kubwa ya pande zote zinazohusika ikiwamo BMT kuketi pamoja na pale ambapo kuna ukiukwaji wa kanuni, wadaawa kupewa muongozoo na kurejeshwa kutekeleza/kurekebisha badala ya kuendelea kuchelewesha ama kusitisha mchakato huo. Sisi tunaamini endapo mchakato huo wa mabadiliko utakamilika, klabu nyingi nchini zitafuata mfumo huo na ndipo soka letu litapiga hatua na kufika kule ambapo tulikuwa tukipatamani/kupahitaji kwa muda mrefu.

Hakuna ubishi kuwa, soka ni ajira kubwa kwa vijana nchini na ili kupiga hatua ama kupata maendeleo lengo kupitia sekta hiyo, kunahitaji uwekezaji mkubwa, hivyo hiki ni kipindi cha serikali kutoa sapoti kubwa kwa namna yoyote ile katika kufanikisha mchakato huo wa mabadiliko.

Tunatamani kuona ligi ya Tanzania ikiwa bora zaidi Afrika na pengine miongoni mwa ligi bora duniani ambazo zitavutia wawekezaji wakubwa zaidi kutoka nje, na ili hilo lifanikiwe, serikali inapaswa kusimamia kwa umakini mwanzo huo wa mchakato wa mabadiliko Simba ili kufanikiwa na hatimaye klabu zingine kufuata njia hiyo kama ambavyo Klabu ya Yanga nayo imeanza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Uwekezaji Simba ukikwama, soka la Tanzania pia litakwama jumla

Na Adam Fungamwango

**NIMEKUWA** nikifuatilia sakata la uwezekaji kwenye klabu ya Simba kwa siku hizi mbili tatu, kuhusu sakata la klabu hiyo na Tume ya Taifa ya Ushindani (FCC).

Nimesikiliza redio, nimeangalia televisheni na kusoma mitandao mbalimbali ya kijamii, nikagundua vitu kadhaa. Kuna upande unataka uwekezaji ufanikiwe ili klabu ya Simba ianze kujitegemea yenyewe na kuendeshwa kwa mfumo ya hisa, kufuatia kupata Mwekezaji, Mohamed "Mo" Dewji.

Wanachama na mashabiki wa Simba wanaamini kuwa Dewji kwa sasa ndiye mtu sahihi kwenye klabu yao anayeweza kuitoa sehemu moja na kuipeleka sehemu nyingine na klabu yao ikaendeshwa kisasa na kuwa mfano ya klabu zingine Tanzania. Lakini suala hili linaonekana kama vile kuna watu nyuma ya pazia, wana mpango wa kutaka kulikwamisha.

Hii imetokana na taarifa iliyotolewa na FCC hivi majuzi, ambayo ilikuwa ikikanusha madai yaliyokuwa yakitolewa na baadhi ya viongozi wa klabu hiyo kuwa wao ndiyo wanakwamisha mabadiliko ya mfumo kwenye klabu hiyo. FCC walikuwa wakijibu madai ya Mo na Mkuu wa Idara ya Habari wa klabu hiyo, Haji Manara, ambao kwa nyakati tofauti, walinukuliwa wakisema kuwa wanachosubiri ni ruhusa kutoka kwa tume hiyo ili mchakato wa mabadiliko uwe umekamilika.

Tume hiyo ni Taasisi ya Serikali iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani namba 8 ya mwaka 2003, ili kusajiisha na kulinda ushindani na biashara na kuwalinda walaji dhidi ya mienendo isiyo ya haki na ya kupotosha.

Sitaki kuingia sana ndani, kuangalia nani kasema nini na nani kajibu nini, lakini suala hili linaonekana kukuzwa bila sababu yoyote ile. Lengo hapa ni kuisaidia Simba kutoka hapa ilipo na kwenda kwenye mabadiliko. Ikumbukwe kuwa kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, hakuna klabu yoyote ambayo imeshawahi kutoka kwenye mfumo wa wanachama na kuingia kwenye hisa na uwekezaji, hivyo hata FCC yenyewe inajifunza kupitia hili. Ni wajibu wa tume hiyo na viongozi wa Simba kukaa pamoja kwa lengo la kulitatua suala hilo na si kuonekana kama kutaka kulifanya liwe gumu na kuleta taharuki kwa mashabiki na wadau wa soka nchini.

Hata kama kuna makosa ambayo Simba wameyafanya, tume ilipaswa kuwaita na kuwaambia mapungufu yote yanayotakiwa kufanyiwa kazi ili mchakato usonge mbele. Kuhusu upatikanaji wa Ofisa Mtendaji kwenye klabu ya Simba, ikumbukwe kuwa Simba bado si kampuni, ila ni klabu ya kucheza mpira, hivyo kabla ya mabadiliko ilikuwa ni lazima iwe na viongozi kwa matakwa ya Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) na hata Shirikisho la Soka Tanzania (TFF). Hakuna klabu ya soka inayoruhusiwa kucheza mpira bila ya kuwa na viongozi, hivyo Simba waliona wasisubiri kwanza, bali wapate viongozi waendelee kuongoza wakati mchakato unaendelea.

Ikumbukwe kuwa mashabiki wengi wa soka Tanzania wamechoshwa na soka la ubabaishaji na wanachotaka ni kuona klabu hizi zikiendeshwa kwa mfumo ambao Simba inataka kuelekea. Klabu zote nchini, ikiwamo hata Yanga kwa sasa darasa lao la mfano ni Simba. Wote wanaiangalia. Itakapofanikiwa na kuingia kwenye mfumo, basi klabu zote zitafuata njia hiyo, tena wao hawatochukua muda mrefu kwa sababu njia yote imeshawekwa na mtangulizi. Lakini kama wapo watu wanataka kufanya mchakato huo uharibike kwa makusudi yao binafsi, basi wajue hawaikomoi au kuiangusha Simba, bali wanaliangusha soka la Tanzania.

Mchakato wa Simba ukifelishwa, labda kwa sababu tu za kukomoana, au Usimba na Uyanga, basi hata Yanga na klabu zingine hazitofanya mabadiliko na soka litarudi kule kule.

Uwapo wa watu wanaojitokeza kuweka kama Mo Dewji, ndiyo umeisababisha hata Yanga kuchangamka na kumpata GSM, badala ya kuendeleza bakuli lao, hivyo kumekuwa na upinzani mkali kwa sasa ambao unainua zaidi soka la Tanzania.

Kwa sasa Ligi ya Tanzania ndiyo inayotazamwa sana Afrika Mashariki na Kati kutokana na kukusanya wachezaji kutoka ukanda wote huo. Na hiyo yote ni kwa sababu ya watu wachache tu walioamua kutaka kuwekeza kwenye soka, Said Salim Bakharesa, Mo na GSM.

Wachezaji kama Clatous Chama, Luis Miquissone, Mukoko Tonombe, Tuisila Kisinda, Prince Dube, Meddie Kagere ni baadhi ya nyota wa kigeni wenye thamani kubwa, wanaofanya ligi ya Tanzania iangaliwe sana Afrika Mashariki na Kati, hivyo wakitumiwa vema wataiingizia Tanzania mapato makubwa kuliko inavyodhaniwa.

# Watakiwa kupeleka malalamiko ya vifungashio TBS, NEMC

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU tatu baada ya kutolewa hadi tarehe 31, Desemba mwaka huu, kuwa mwisho wa utumiaji wa vifungashio vya maji, chupa na biashara mbalimbali zinazofanywa na wachuuzi, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limewataka wale wenye malalamiko au ushauri zaidi kuwasiliana na baraza hilo au Shirika la Viwango la Taifa (TBS).

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, NEMC ilisema tangu katazo la uzalishaji, usambazaji na matumizi ya plastiki Juni 30, 2019 lifanikiwe, kumekuwa na ongezeko la matumizi ya vifungashio vya plastiki mitaani na kutishia athari za mazingira.

"Lengo letu ni nzuri na linalenga kuhakikisha kuwa sheria na taratibu zote za kimazingira zinafuatwa na kulindwa wakati wote. Na tunategemea wazalishaji watakaoathirika watawasilisha malalamiko yao," imesema taarifa hiyo.

ongezeko la uzalishaji wa vifungashio vya plastiki ambavyo chanzo chake hakijulikani na pia vifungashio ambavyo havina kibali cha TBS ni hatari kwa afya ya binadamu na mazingira yake.

Taarifa ya baraza ilisema kuwa utengenezaji, usambazaji na matumizi ya vitu hivyo ni uvunjaji wa Kanuni Na 3 na 4 za Sheria ya Mazingira ya 2004, kanuni ambazo zilitungwa na kutangazwa 2019 ili kutekeleza katazo la serikali la matumizi ya plastiki.

Kanuni namba 3 inawataka wazalishaji kuwa na kibali kutoka TBS baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa, lakini kinachoonekana kwa sasa taratibu hizo hazifuatwi wala kuheshimiwa.

Aidha, katika taarifa hiyo, NEMC imesisitiza kuwa kama msimamizi wa mazingira haitakuwa tayari kuona uzalishaji holela wa vifungashio usiozingatia kanuni na taratibu za kimazingira unaendelea.

Taarifa iliongeza kuwa kuwapo kwa vifungashio visivyokidhi viwango sokoni ni kinyume cha Kanuni ya 4 (b) na (c) ambayo imetungwa na kutangazwa ili kulinda afya ya binadamu, wanyama pamoja na mazingira dhidi ya athari zinazoweza kujitokeza.

Tangu katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki, vikundi 2,761 vya watengenezaji wa mifuko mbadala vimeanzishwa na kutengeneza ajira nyingi kwa Watanzania. Sambamba na hilo NEMC imeshachukua hatua mbalimbali kutoa elimu kwa wadau na wananchi umuhimu wa matumizi ya vifungashio mbadala.

NEMC imeendelea kuwaomba Watanzania kushirikiana na baraza kutoa taarifa za watengenezaji wa vifungashio visivyoruhusiwa ili kuchukua hatua stahiki zinazofaa kisheria.




Mkurugenzi wa Usalama na Afya kutoka Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) jijini Arusha, Mhandisi Alex Ngata, akizungumza jana jijini humo na wafanyakazi kutoka sehemu mbalimbali (hawapo pichani) wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya Vision Zero yaliyoandaliwa na wakala huyo yenye lengo la kuwapa elimu ya kujikinga dhidi ya magonjwa na ajali zinazotokea maeneo ya kazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mradi usimamizi misitu shirikishi mbioni

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI kupitia kwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) na wadau mbalimbali wa sekta ya misitu, wameandaa andiko la mradi wa usimamizi shirikishi wa misitu ya miombo ya nyanda za Tanzania.

Mradi huo utafadhiliwa na Mfuko wa Mazingira Duniani awamu ya saba (GEF-7), unalenga kuondoa na kuzuia uharibifu wa ardhi na upotevu wa bionuai katika ikolojia ya misitu ya miombo ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni mikoa ya Katavi, Rukwa na Songwe na Kanda ya Magharibi ambayo ni Mkoa wa Tabora.

Akizungumza katika mkutano wa kuhakiki mradi huo, ulioshirikisha wataalamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Rais, FAO, wakurugenzi wa wizara, taasisi na halmashauri pamoja na wadau wa maendeleo, Kamishna wa Uhifadhi Misitu, Tanzania, Profesa Dos Santos Silayo, alisema unatarajia kughalimu dola za kimarekani milioni saba. Kamishna Prof. Silayo alisema mradi huo utatekelezwa katika awamu kadhaa ambapo awamu ya kwanza utaanza kati ya Wilaya Mlele (Katavi) na Kaliua Tabora ambayo utasaidia kuzuia ardhi na upotevu wa bionuai katika ikolojia ya misitu ya miombo.

"Awamu ya kwanza mradi utalenga ukanda wa North Ugala-Mpanda line - Isawima Landscape katika wilaya za Kaliua na Rungwa River-Mlele Hills - Inyonga Landscape katika wilaya ya Mlele, lakini baadaye mradi utaendelea na wilaya nyingine," alisema Prof. Silayo.

Naye Mhandisi Geofrey Bakanga, kutoka FAO, alisema umuhimu wa misitu ni suala ambalo lipo wazi kwa kila mmoja kutokana na maisha ya kila mwanadamu yanategemea uwapo wa misitu kutokana na huduma muhimu za mazingira na kusaidia upatikanaji wa chakula.

Hata hivyo, alisema misitu imekuwa ikipotea kwa kiwango cha kushangaza ulimwenguni kwani inakadiriwa kuwa karibu hekta milioni 7.3 hupotea kila mwaka na Afrika ndio inaongoza kwa upotevu na uharibifu unaokadiriwa kufikia hekta milioni 3.94 katika kipindi cha mwaka 2010 - 2020.

Alisema kutokana na kuwepo kwa changamoto hiyo, mfuko wa dunia wa kuhifadhi mazingira umelenga kusaidia nchi zinazoendelea kutatua tatizo hilo kwa kuja na mpango maalumu wa kuonyesha matokeo unaozingatia ujumuishi wa usimamizi wa misitu kupitia kanda za uzalishaji kisekta.

Naye mratibu wa mradi huo ambaye ni Ofisa Misitu Mkuu kutoka TFS, Zainabu Bungwa, alisema mradi huo utakuwa wa miaka mitano ili kutatua changamoto zinazozunguka jamii kwa kuwa misiti ya miombo imekuwa ikibeba jamii za aina zote ikiwamo wafugaji, wakulima, wafugaji wa nyuki na wananchi wanaoshughulika na dawa za asili, ambao wamekuwa wakifanya matumizi yasiyo endelevu kutokana na shughuli za kibinadamu.

## Ajali za kitabia zapunguza ari kujisomea

**Na Saada Akida**

KUTOJUA matumizi sahihi ya lugha ya kufundishia na ajali za kitabia zitokanazo na kundi rika, zimetajwa kuwa miongoni mwa vikwazo vinavyochangia kupunguza ari ya kujisomea na kuporomosha kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa sekondari.

Hayo yameelezwa na Mkurugenzi wa Shule Huria ya Ukonga Skillful, Diodorus Tabaro, wakati wa mahafali ya kidato cha nne na QT yaliyofanyika Ukonga Magereza jijini Dar es Salaam.

Katika mahafali hayo, alifichua namna shule hiyo ilivyopambana na ajali za kitabia pamoja na mikakati ya kuzitokomeza.

Tabaro ambaye kitaaluma ni mwalimu, alisema kwa kuzitambua changamoto hizo, imekuwa rahisi kwa shule yake kukabiliana nazo na kwamba wamejipanga kuzitokomeza kabisa katika mwaka ujao wa masomo na kupandisha ufaulu Ukonga Skillful Open School.

"Tumejielekeza katika kuziba mianya inayostawisha wanafunzi kuathiriwa na kundi rika, huku shule ikitoa mafunzo ya ziada ya lugha ya kufundishia yaani Kiingereza (English Course)," alisema na kuongeza:

"Mambo ambayo yamekuwa ndio siri ya ufaulu mzuri hapa Ukonga Skillful Open School, ambako mwaka jana tulifaulisha kwa asilimia 90 ya wahitimu na wakajiunga vyuo vikuu mbalimbali nchini."

Naye mgeni rasmi wa mahafali hayo yaliyohusisha wanafunzi 115, Bryceson Makena, aliwataka wazazi na walezi kuacha kusingizia utandawazi wanapokwama katika kuwajenga watoto wao kimaadili na kuwa sababu ya wengi wao kufeli ama kukatiza masomo.

Makena, ambaye ni Mwalimu, Mshereheshaji na Mhamasisaji maarufu nchini, alisema siri pekee ya kutokomeza kundi rika miongoni mwao wanafunzi ni wazazi na walezi kujikita katika malezi bora, yanayohusisha mafunzo ya imani za kidini.

"Mzazi ni figa kuu na muhimu katika mafiga matatu yanayoelezwa na falsafa kongwe ya elimu. Wazazi wasisingizie utandawazi, kwani wapo vijana wanaomudu kulikwepa kundi rika, kutokana na msingi imara wa malezi waliopewa nyumbani," alisema Makena.

Alibainisha kuwa wanapokwama wazazi nyumbani katika kuwajenga watoto, kazi huwa ngumu kwa walimu shuleni na akiipongeza Ukonga Skillful Open School kwa namna ilivyofanikiwa kubadili fikra za wanafunzi waliokosa alama za kutosha shuleni mwao na kufeli, kuwa wasomi wazuri wanaofaulu kwa alama za juu shuleni hapo.

# Mtaalamu aeleza chanzo mfumuko wa tope Dar

**Na Elizabeth Zaya**

MTAALAMU wa miamba kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Hudson Nkotagu, ameeleza sababu zinazochangia kutokea hali ya mfumuko wa tope juu ya ardhi katika eneo la Kunduchi Mtongani, jijini.

Akizungumza na Nipashe jana, Prof. Nkotagu, alisema hali hiyo husababishwa na mambo mbalimbali, ikiwamo hali ya kiasili kama kutokea matetemeko, shughuli za kibinadamu ikiwamo za kutumia baruti na ardhi kujaa maji.

Hivi karibuni, hali hiyo ya mfumuko wa tope ilitokea katika eneo la Kunduchi, Mtongani, Kinondoni jijini Dar es Salaam ukizingira nyumba za wakazi wa eneo hilo na kuzua taharuki.

Alisema hali hiyo inapotokea, huwa ipo haja ya kutumia wataalamu kuzuia athari zaidi.

"Hali hiyo inaweza kutokea endapo kuna shughuli za kibinadamu zinafanyika hapo hususani za uchimbaji wa kutumia baruti. Pia kama eneo hilo ni la mchanga halafu ardhi ikajaa maji yanayotokana na kunyesha kwa mvua nyingi ambayo siyo ya siku moja halafu matetemeko makubwa au madogo yasiyosikika kiurahisi," anasema Profesa Nkotagu.

"Na ardhi ikishajaa maji mengi, kule hutengeneza uji ambao katika eneo hilo kama kuna mahali penye ufa kidogo ndipo hapo uji hutokea mpaka uishe wote na hutegemea ni mwingi kiasi gani."

Kwa mujibu wa Prof. Nkotagu, baada ya kutokea kwa hali hiyo, eneo hilo huwa siyo salama sana kwa kutumiwa na watu kwa sababu huwa tayari ni teke na linakuwa limedidimia.

"Kwa hiyo ni hatari hata kwa mtu kukanyaga kwa sababu linakuwa ni teke na limedidimia, sasa ikitokea mtu akikanyaga wakati mwingine anaweza kudidimia na akapata madhara," alisema.

"Ili kuwa salama linatakiwa lipimwe kitaalamu na kujua ukubwa wa eneo lililoathirika na limedidimia kiasi gani."

**HALI HIYO INAZUILIKA**

Prof. Nkotagu alisema zipo njia nne za kuzuia athari zaidi katika eneo ambalo kumetokea hali hiyo ikiwamo kupanda miti aina ya mikaratusi ambayo hunyonya maji kwa kiwango kikubwa, kunyonya maji, kuchimba mirefeji au kuchimba visima.

**RC ATOA AGIZO WAKAZI KUHAMA**

Jana Mkuu wa Dar es salaam, Aboubakar Kunenge, aliwataka wakazi wa eneo hilo kuhama mara moja wakati serikali inaendelea kufanya utafiti kujua ukubwa wa eneo lililoathirika.

Kunenge akiongozana na wajumbe wa kamati ya usalama ya mkoa walifika katika eneo hilo kushuhudia uwapo wa tope hilo ambalo pia limesababisha baadhi ya nyumba na mifugo kutitia, kupasuka nyufa.

Kunenge alimwagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni kuweka alama za hatari katika eneo hilo wakati serikali chini ya taasisi ya Geologia na utafiti ya madini Tanzania ikiendelea kutafiti ukubwa wa eneo lililoathirika.

Alisema serikali inaangalia utaratibu wa kuwapatia wananchi wa eneo hilo viwanja vingine, ili waendelee na maisha kama awali.

Awali, mtafiti kutoka taasisi ya Geologia na utafiti wa madini, Gabriel Mbogoni, alisema matokeo awali yamebaini kwamba chanzo cha tope kuharibika na kusababisha tope ambalo linasukumwa kutoka chini kwenda kwenye uso wa ardhi.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Renatus Mchau, akipokea msaada wa madawati 100 kutoka kwa Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango (kulia), msaada huo ni kwa ajili ya Shule ya Msingi Kipindimbi wilayani humo, baada ya kuwa na ongezeko la wanafunzi kutokana na kufungwa kwa Shule ya Msingi Njinjo iliyokumbwa na mafuriko mwanzoni mwa mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwalimu mbaroni madai ya kujeruhi akigombania pombe

**Na Said Hamdani**, LINDI

MKULIMA na mkazi wa Kijiji cha Turuki, Kata ya Mihumo, Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, Said Amani Mikunya (25) amelazwa katika Hospitali ya Wilaya hiyo, akidaiwa kujeruhiwa kwa panga na mwalimu kwenye kilabu cha pombe.

Mikunya anadaiwa kujeruhiwa na mtumishi huyo wa serikali, Sudi Juma Sufiani (31), walipokuwa wakigombea pombe ya moshi (gongo).

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, Foka Dinya, alisema tukio hilo linadaiwa kufanywa na mwalimu huyo, Ijumaa majira ya asubuhi.

Alisema siku hiyo wakiwa na wenzao wakipata kinywaji hicho, Sufian anadaiwa kuchukua pombe ya Mikunya ili anywe bila ya ridhaa yake, kitendo ambacho kilikataliwa na Mikunya, ndipo ugomvi ulipoanza.

Dinya alisema katika purukushani hizo za kugombea pombe, pembeni kulikuwa na panga ambalo mtuhumiwa anadaiwa kulitumia kumjeruhi Mikunya kwenye mguu wake wa kushoto sehemu ya chini ya goti na kumsababishia jeraha lililoambatana na maumivu makali kwenye mwili wake.

"Watu hawa walikuwa wanakunywa pombe aina ya gongo...sasa huyu mtuhumiwa ambaye ni mwalimu wa shule ya msingi alichukuwa pombe ya Mikunya bila ya ridhaa yake na ndipo ugomvi ulipoanza," alisema Kamanda Dinya.

Alisema baaada ya kitendo hicho, watu waliokuwapo kwenye eneo hilo waliingilia kati kwa kuwakamata na kuwafikisha Kituo cha Polisi Liwale Mjini. Dinya amesema Mikunya kwa sasa amelazwa Hospitali ya Wilaya ya Liwale, akiendelea kupatiwa huduma za matibabu kwa majeraha na maumivu aliyoyapata, na kueleza kuwa hali yake inaendelea kuimarika.

Amesema mwalimu huyo naye licha ya kupata maumivu kwenye mwili wake, atafikishwa mahakamani kujibu shtaka baada ya kukamilisha uchunguzi na taratibu zingine za kiofisi. Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Liwale, Dk. Kweyombo, alithibitisha kumpokea majeruhi na kueleza kuwa hali yake inaendelea kuimarika, kutokana na matibabu anayopewa.

# Vyeti kuanza kutolewa baada ya kuzaliwa 2022

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), umesema kufikia mwaka 2022 watoto wote wanaozaliwa nchini watakuwa wanapata vyeti vya kuzaliwa mara tu wanapozaliwa.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu, Emmy Hudson, alisema RITA imepanga kutekeleza hilo kutokana maboresho makubwa katika mfumo wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu hususani katika usajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto kupitia mpango wa usajili wa watoto walio na umri chini ya miaka mitano.

Alisema mpango huo umeanza na unatekelezwa katika mikoa 18 nchini na kwamba mpaka 2022 utekelezaji katika mikoa nane iliyobaki utakuwa umekamilika.

"Mpango wa usajili wa watoto umesaidia kugatua majukumu ya usajili na kusogeza huduma hiyo karibu na makazi ya wananchi, ambapo huduma za usajili kwa sasa zinatolewa bila malipo, katika vituo vya Tiba na Ofisi za Watendaji Kata," alisema Hudson.

"Maeneo hayo ni ya kimkakati kwa sababu ni rahisi kwa kila mwananchi kufika na kupatiwa huduma husika. Mtoto anayezaliwa katika kituo cha Tiba anaweza kupata cheti cha kuzaliwa kabla ya kutoka hospitali, cha msingi ni kwa wazazi wenyewe kuandaa jina la mtoto litakalojazwa katika cheti."

Alisema asilimia 13 ya watoto chini ya miaka mitano waliokuwa wamesajiliwa mwaka 2012 walikuwa asilimia 13 tu na kwamba idadi hiyo imeongezeka na kufikia asilimia 49.4 mwaka 2020.

# CCM yapata madiwani viti maalum 1,285

**Na Elizabeth Zaya**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imefanya uteuzi kwa madiwani wa viti maalum 1,348 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika mikoa mbalimbali.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na NEC, na idadi ya madiwani kwa kila mkoa ilionyesha kuwa Arusha (54), Dar es Salaam (36), Dodoma (71), Geita (43), Iringa (37), Kagera (64) na Katavi (18).

Mikoa mingine ni Kigoma (43), Kilimanjaro (59), Lindi (49), Manyara (50), Mara (59), Mbeya (59), Morogoro (73), Mtwara (59) na Mwanza (66).

Mingine ni Njombe (36), Pwani (46), Rukwa (30), Ruvuma (56), Shinyanga (45), Simiyu (46), Singida (48), Songwe (32), Tabora (73) na Tanga (82).

Kwa mujibu wa NEC, madiwani waliopaswa kupigiwa kura Oktoba 28 mwaka huu ni 5,350, lakini katika hatua za awali CCM ilipata madiwani 870 waliopita bila kupingwa.

Hadi sasa kuna kata tatu zitafanya uchaguzi Desemba, kutokana na kutofanya uchaguzi kwa sababu mbalimbali huku kata nne madiwani wateule walifariki dunia.

# Umeme jua wapunguza vifo vya mama, mtoto

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

UFUNGAJI wa umeme jua katika Kituo cha Afya cha Mwamgongo kinachohudumia zaidi ya watu 54,000, umesaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto katika ukanda wa Ziwa Tanganyika ambao haufikiki kirahisi isipokuwa kwa njia ya maji pekee.

Kutokana na eneo hilo kutokuwa na nishati ya umeme, awali wajawazito waliohitaji kufanyiwa upasuaji walilazimika kusafirishwa kwa njia ya maji kwa takribani saa tatu kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kigoma Maweni, hali ambayo ilisababisha wengi kupoteza maisha wakiwa njiani .

Mfumo huo wa umeme wa jua umetekelezwa na Shirika la World Vision Tanzania chini ya ufadhili wa serikali ya Canada kupitia mradi wa Sustain Kigoma, baada ya kubaini afya ya mama na mtoto kuwa hatarini.

Akikabidhi mradi huo kwa serikali Meneja wa mradi Sustain Kigoma, Dorothea Sago, alisema kutokana na kituo hicho kuwa pekee kinacho tegemewa na ukanda wa mwambao wa Ziwa Tanganyika, walitekeleza mradi ili uwe msaada kwa wananchi wanaoishi mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Alisema takribani shilingi milioni 315 zimetumika kukamilisha ufungaji nishati hiyo kwenye kituo cha afya na nyumba 10 za wafanyakazi, hatua ambayo imeboresha mazingira ya utoaji huduma kwani huduma zote muhimu ambazo awali zilikuwa hazifanyiki, zimeanza kutolewa.

Mganga Mawidhi wa Kituo cha Afya cha Mwamgongo, Hamis Said, alisema Februari mwaka huu ndipo huduma zinazotegemea nishati hiyo zilianza kufanyika ikiwamo upasuaji na uhifadhi wa damu salama na kusaidia kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 9 kwa mwaka jana hadi 2 kuanzia Januari hadi Novemba mwaka huu.

"Sisi usafiri wetu pekee ni usafiri wa boti kumfikisha mama kwenye huduma inachukua takribani saa tatu hivyo vifo vingi vilikuwa vinatokea ziwani wakielekea kwenye huduma," alisema.

Alex Ntiboneka, mwakilishi Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, alisema kwa mwaka 2020 serikali ilipeleka shilingi milioni 400 kuboresha majengo katika kituo hicho ambacho awali kilikuwa zahanati na ufungwaji wa umeme uliofanywa na wadau umeipunguzia gharama serikali ya usafirishaji wagonjwa.

Fransio Kindo, mwanamke aliyefanyiwa upasuaji katika kituo hicho, alisema sasa hawana wasiwasi tena wanapopata ujauzito kwani huduma za dharura zinazotegemea nishati ya umeme kama upasuaji zinafanyika.

Wajawazito 22 wamefanyiwa upasuaji hadi sasa tangu huduma hiyo kuanza mapema mwaka huu.




Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni na Mkurugenzi wa Biashara Vodacom Tanzania PLC, Linda Riwa, wakizindua rasmi promosheni mpya ya Shangwe Shangwena jana, inayoendana na maadhimisho ya miaka 20 ya Vodacom na msimu huu wa sikukuu wateja wa M-Pesa watajishindia magari matano aina ya Renault Kwid na zawadi mbalimbali za Sh. bilioni 3. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge ataja mambo saba ya kipaumbele

**Na Augusta Njoji,** IKUNGI

MBUNGE wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, ametaja mambo saba atakayosimamia kwa kipindi cha miaka mitano, huku akiahidi kuwatumikia wananchi bila kuwabagua kwa itikadi zao za kisiasa.

Jimbo hilo katika miaka tisa iliyopita lilikuwa chini ya upinzani ambapo lilikuwa likiongozwa na Tundu Lissu.

Akizungumza jana alipokuwa akipokelewa na wananchi wake na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutoka Bungeni Dodoma, Mtaturu alisema uchaguzi umekwisha, hivyo wananchi washirikiane kuhakikisha Wilaya ya Ikungi inapata mafanikio na yeye kama kiongozi wao atawatumikia wote bila ubaguzi.

"Mimi ni mbunge wenu nipo tayari kushirikiana nanyi, lakini tujenge uhusiano, tuachane na itikadi zetu za kisiasa sasa tujenge uchumi wa Jimbo la Ikungi, tumechelewa sana," alisema.

Akizungumzia kuhusu vipaumbele, Mtaturu alisema atatekeleza vipaumbele saba likiwamo suala la elimu ambapo atasimamia kuhakikisha watoto wanapata elimu bora.

"Nitajenga miundombinu nitasimamia vyema mitaala nikiwa bungeni ili elimu inayotoka imsaidie mtoto, kama nilivyoanza nilihakikisha Chuo cha VETA kinapatikana na sasa kipo katika hatua za mwisho kukamilika," alisema.

Alisisitiza ataendelea kutoa sare za shule kwa wanafunzi wasio na uwezo wanaoanza shule wa darasa la kwanza na kidato cha kwanza.

Aidha, alisema kipaumbele kingine ni suala la afya ambapo atahakikisha maeneo yasiyo na vituo vya afya na zahanati vinajengwa ili kusogeza huduma za afya kwa wananchi wa jimbo hilo.

"Kipaumbele kingine ni maji nitahakikisha miradi iliyopo inatekelezwa na kuibua mingine ili wananchi wapate majisafi na salama kwa asilimia 100," alisema.

Kuhusu umeme, alisema ndani ya miaka mitano atahakikisha vijiji na vitongoji ambavyo havina umeme vinapata ili kuchochea maendeleo ya jimbo hilo.

"Miundombinu tutahakikisha barabara zinaboreshwa na watu wanakwenda kupata huduma bila kikwazo," alisema.

Kadhalika, alisema atahakikisha anasimamia uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuwaomba wananchi kuunda vikundi ili kupata fursa za mikopo kwa kuwa vikundi vinaleta nidhamu ya fedha.

"Ule mradi wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe unakwenda kutekelezwa sasa wale watu 20 wa kwanza ambao vibanda vipo tayari watapatiwa, madiwani hamasisheni wananchi, nipo tayari kuleta ng'ombe tufuge kisasa tubadilishe uchumi wa jimbo letu, pia nitasimamia michezo na kuendeleza vijana wenye vipaji," alisema.

Aliwahamasisha kinababa kuunda vikundi vya wakulima, ili kupata mikopo itakayosaidia kuinua kilimo chao.

## Kilwa yapigwa jeki elimu, afya

**Na Said Hamdan,** LINDI

WILAYA ya Kilwa mkoani Lindi imepewa msaada katika sekta ya afya na elimu wa Sh. milioni 12.5.

Msaada huo umetolewa na Benki ya NMB ukiwa ni urejeshaji wa faida ya benki hiyo kwa umma. Kwa mwaka huu benki hiyo imetenga zaidi ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya kusaidia jamii. Akikabidhi misaada hiyo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Renatus Mchauru, Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango, alisema benki imewiwa kutoa misaada hiyo baada ya kuombwa na jamii. Alisema wakati anapata matibabu katika Kituo cha Afya Masoko, alibaini hitilafu zilizokuwapo katika kituo hicho na alipozungumza na utawala walimweleza tatizo na kuwashauri waandike barua ya kujieleza, kitu ambacho walifanya.

Alisema Benki ya NMB imekarabati jengo la baba, mama na mtoto kwa kuweka paa jipya, kupaka rangi na kuweka michoro ambayo inaleta taswira njema kwa wadau wanaofuata tiba.Alisema benki hiyo inaona fahari kusaidia eneo hilo ili liwe rafiki kwa wahitaji. Alisema kazi ya kukarabati jengo hilo la hospitali katika Kituo cha Afya Masoko uligharimu Sh. milioni 2.5. Naye Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, John Nkuba, alishukuru benki hiyo kwa msaada wake na kusema mazingira ya matibabu sasa baada ya ukarabati huo yako bora zaidi.

Alisema kituo hicho kinachohudumia watu 50 kwa siku bado kinahitaji pia mashuka, vitanda na nishati mbadala. Mkurugenzi Mchauru pamoja na kushukuru kwa misaada hiyo, aliwataka watumishi kuhakikisha wanatoa huduma nzuri na bora zaidi kulingana na uzuri wa majengo yaliyopo sasa.

Akizungumza wakati wa kukabidhi madawati katika Shule ya Msingi ya Msingi Kipindimbi, Shango alisema wametoa madawati 100 kwa ajili ya wanafunzi wapya wa shule hiyo.

Shule hiyo iliyokuwa na madawati 100 ilizidiwa baada ya wanafunzi kuongezeka kufuatia maafa ya mafuriko yaliyokumba shule na makazi katika kata ya Njinjo mwanzoni mwa mwaka huu. Shule hizo ni pamoja na Njinjo na Ndende. Maafa hayo yaliyokumba watu zaidi ya 6,804 katika kata ya Njinjo yalisababisha Shule ya Kipindimbi wanafunzi wake kuongezeka kutoka watoto 400 hadi 909 na kusababisha upungufu wa madawati zaidi ya 100.

Katika hafla zote mbili Shango alishauri wazazi kuanza mapema kuwafunza watoto wao kuweka akiba kwa kuwafungulia akaunti watoto wao ili waweze kuja kujisaidia siku za baadaye.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Bahati, alisema pamoja na kusaidiwa madawati hayo, shule hiyo bado inakabiliwa na tatizo la matundu ya choo kwa wanafunzi na walimu na pia nyumba za walimu.

## Shule yapewa saruji tani nne ujenzi wa madarasa matano

**Na Mwandishi Wetu,** BUKOBA

SHULE ya Msingi Ibosa iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, imepewa tani nne za saruji kwa ajili ya ujenzi wa madarasa matano.

Msaada huo ulitolewa na benki ya NBC kama sehemu ya urudishaji kwa jamii, ambapo utasaidia kufanya maboresho ya miundombinu ya madarasa na hatimaye kupunguza msongamano wa wanafunzi unaoikabili shule hiyo hivi sasa.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Meneja wa NBC tawi la Bukoba, Mathias Muhangirwa, alisema mchango huo utasaidia katika kuboresha miundombinu ya madarasa, ili kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu katika mazingira bora.

Aidha, alisema ili mpango wa serikali wa utoaji elimu bure ufanikiwe ni lazima wadau mbalimbali wajitokeze kuchangia katika ujenzi wa miundombinu kama madarasa lengo likiwa ni kukidhi mahitaji ya wanafunzi wanaojitokeza kuanza darasa la kwanza kila mwaka.

"Kama sehemu ya urudishaji kwa jamii tumeona ni vema kuunga mkono jitihada hizi za uboreshaji wa miundombinu kwa kutoa tani nne za saruji ambazo tunaamini zitasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani," alisema meneja huyo.

Akipokea msaada huo, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, Babylus Mashauri, alisema kwa sasa shule hiyo ina wanafunzi 789, ambapo kwa mujibu wa taratibu za wizara ya elimu shule hiyo ilibidi iwe na madarasa 14 ingawa yaliyopo sasa ni tisa.

"Tuna upungufu wa vyumba vitano kwa hiyo unaweza kuona jinsi kulivyo na msongamano kwenye madarasa hayo, kwa msaada huu utakuwa ni chachu ili tuweze kuongeza vyumba ili kukidhi mahitaji ya shule hii," alisema.

# Mnada wanufaisha wakulima korosho

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

WAKULIMA wa korosho katika wilaya za Mkuranga, Kibiti na Rufiji, wameuza zao hilo, kwa njia ya soko la bidhaa Tanzania (TMS).

Akizungumza baada ya kufanyika mnada huo, Kaimu Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika Mkoa wa Pwani (CORECU), Ally Sultan Mingesi, alisema korosho zote za daraja la kwanza na la pili zimeuzwa kwa bei tofauti kulingana na madaraja.

"Daraja la kwanza katika Wilaya ya Mkuranga limeuzwa kwa kilo Sh. 2,000 huku la pili likiuzwa kwa Sh. 1,430 kwa kilo," alisema.

Mingesi ambaye ni mkulima wa zao hilo Njopeka Mkuranga, alisema kuwa daraja la kwanza Kibiti liliuzwa kwa kilo shilingi 2020, huku daraja la pili likiuzwa kwa shilingi 1,531.

Aliongeza kwa Rufiji, daraja la kwanza liliuzwa kwa shilingi 1,900 huku daraja la pili likiuzwa kwa shilingi 1,340.

Alisema mnada wa tatu unatarajiwa kufanyika katika Wilaya ya Ikwiriri Novemba 25 , mwaka huu. Meneja wa Bodi ya Korosho tawi la Dar es Salaam, Jafar Mataka, aliwapongeza viongozi wa halmadhauri za wilaya za Mkuranga na Kibiti kwa kufuatilia kwa ukaribu matokeo ya mnada, kitendo ambacho kinaonyesha wanavyofuatilia mapato ya wakulima wao ikiwamo na serikali kwa ujumla.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmadhauri ya Mkuranga, Mshamu Munde, aliwataka maofisa kilimo kutoka kata zote 25, waendelee kusimamia ubora wa korosho kwa kuanzia katika maghala ya vyama vya msingi (AMCOS) hadi korosho zinapoingia ghala kuu Mwandege.




Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Idd Kimanta, akikata utepe kuashiria uzinduzi wa mashine ya kubadili fedha ya Benki ya CRDB. Wanaoshuhudia ni Mkurugenzi wa Usimamizi wa Sekta ya Fedha Benki Kuu, Jerry Sabi (wapili kulia) na Ofisa Mkuu wa Uendeshaji Benki ya CRDB, Bruce Mwile (wa pili kushoto), Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Wakati wa benki hiyo, Boma Raballa (kushoto), Meneja wa Kanda ya Kaskazini, Chiku Issa (kulia). Uzinduzi huo ulifanyika katika tawi la Benki ya CRDB Meru jijini Arusha mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana wajipanga kuongeza vyanzo vya nishati

**Na Christina Haule,** MOROGORO

JUMUIYA ya Vijana ya Shirika la Raleigh Tanzania imejipanga kuongeza matumizi ya vyanzo vya nishati endelevu kwa vijana milioni 10 na taasisi 20 za Tanzania ifikapo Juni mwaka 2022, ili kukabiliana na upotevu wa misitu.

Uharibifu huo unafanywa na wavunaji na wauzaji wa mkaa na kuni kwa ajili ya nishati kwa sasa.

Hayo yalisemwa na Katibu wa Jumuiya hiyo, Elibariki Simon, wakati akimkaribisha mgeni rasmi kuzindua kampeni ya "kesho tutachelewa" iliyofanyika mjini hapa.

Simon alisema vijana milioni 10 wa kitanzania watakuwa wamejiunga na harakati za Jumuiya ya Raleigh Tanzania kupitia kampeni hiyo na kujitolea kuchukua hatua chanya za kimazingira kwa kupanda miti milioni 10 ifikapo mwezi Juni mwaka 2022.

Alisema ili kufikia malengo hayo makubwa wanashirikiana na washirika mbalimbali ikiwamo wadau na sekta za serikali za kimazingira kama vile Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na mashirika mengine binafsi na hivyo kugeuza mienendo hasi ya mazingira na kuwa chanya.

Alisema mabadiliko hayo yatasaidia watunga sera na kutekeleza sera chanya za mazingira sambamba na kuhamasisha kizazi cha vijana wa kitanzania kutenda kazi kwa mustakabali wa kuzingatia uwapo wa kizaji kijacho, jamii na nchi yao kwa ujumla.

Alisema kwa mujibu wa takwimu kutoka sekta ya Maliasili na Utalii, Tanzania inapoteza kiwango cha hekta laki 3-4 za misitu kila mwaka ambayo ni zaidi ya mara mbili ya wastani wa dunia.

Alisema pia suala la uvunaji wa mbao, mkaa na bidhaa zingine za misitu zimesababisha viwango vikubwa vya kugawanywa na uharibifu, ambapo kati ya mwaka 2001 na 2015 hekta milioni 1.8 za ardhi zilipotea kwa ripoti ya Umoja wa Mataifa (UN).

Alisema Tanzania ikiwa na zaidi ya theluthi mbili ya idadi ya vijana chini ya umri wa miaka 25, ambapo fursa za kuhamasisha kizazi cha vijana katika kuunda Tanzania ya kijani bado hazijawa kubwa zaidi.

Naye Mratibu wa mradi wa Jumuiya ya Vijana wa Raleigh, Gerald Tupa, alisema jumuiya hiyo ina zaidi ya vijana 1,000 kutoka mikoa mbalimbali Tanzania walio katika maeneo mbalimbali kikanda.

Alisema katika mwendelezo wa kampeni ya upandaji miti jumla ya miti 40,000 ilipandwa tangu 2016 hadi 2017katika mikoa ya Morogoro, Arusha, Mwanza na wilaya zake.

Mmoja wa wajumbe hao, Regina Mmasi, alisema tangu kuanza michakato ya kampeni hiyo, vijana wengi wamepata hamasa ya kuendelea kujishughulisha kwenye shughuli za kijamii sambamba na kuleta mwamko zaidi kwa vijana.

Akifungua kampeni hizo Kaimu Ofisa Mazingira Manispaa ya Morogoro, Alex Roman, aliwataka wadau wengine wa mazingira kujitokeza katika upandaji miti kwa sababu maeneo bado yapo mengi.

Nipashe
Spotika



MABEKI 10 WALIOFUNGA MABAO MENGI KARNE 21 UK. 12-13




# MAKOCHA WA5 WALIOKALIA KUTI KAVU ULAYA HADI SASA

**LONDON,** England

PENGINE ni kazi mbaya zaidi na yenye siri ya aina yake kwenye soka, kwani wakati timu inapofanya vibaya mara zote, kocha ndiye anayebebeshwa mzigo wa lawama kwa kiwango kibovu cha klabu.

Huku msimu wa 2020-21 ukiendelea, makocha kadhaa katika ligi tano kubwa Ulaya wanaweza kupoteza kazi zao kutokana na viwango tofauti vya timu zao.

Makala haya yanawaangalia makocha watano ambao wanaweza kufukuzwa kazi katika klabu zao kabla ya mwishoni mwa msimu huu, hawa hapa...

### #5. Antonio Conte (Inter Milan)

Msimu uliopita, Antonio Conte alionyesha kiwango cha kuvutia pale Inter Milan ambao walipitwa pointi moja tu na Juventus waliotwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, na pia wakatinga fainali ya Ligi ya Europa.

Hata hivyo, kocha huyo wa zamani wa Juventus, ameshindwa kuendelea na kiwango kile msimu huu, huku Inter wakiwa nafasi ya saba kwenye msimamo wakipitwa pointi tano na vinara AC Milan.

Hata kwenye Ligi ya Ulaya, vijana hao wa Conte wapo kwenye wakati mgumu, kwani Inter inashika mkia kwenye kundi lake la Ligi ya Mabingwa Ulaya ambalo lina timu za Bayer Leverkusen, Shakhtar Donetsk na Real Madrid.

### #4. Andrea Pirlo (Juventus)

Ni moja ya mwanzo mbaya zaidi wa Serie A kwa Juventus katika misimu ya hivi karibuni, kwani wamepitwa pointi nne na vinara AC Milan wanaoongoza msimamo baada ya mechi saba.

Bianconeri hao walianza maisha mapya msimu huu chini ya kocha mpya, Andrea Pirlo na walionekana kuwa na mwanzo mzuri kwa kushinda mechi yao ya kwanza, lakini baadaye mambo yakaanza kuonekana kuwa magumu. Mabingwa hao wa Serie A walifungwa mabao 2-0 na Barcelona kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na sasa ni wazi kwamba nafasi ya Pirlo inaanza kuzua maswali.

Licha ya kiwango bora cha Alvaro Morata, Juventus na Pirlo bado wanaonekana kusuasua pamoja na uwapo Cristiano Ronaldo.

### #3. Ronald Koeman (Barcelona)

Ronald Koeman alipewa mikoba ya kuinoa klabu hiyo, baada ya kuwa na msimu mbaya zaidi uliopita kwa kipindi cha muongo mmoja.

Baada ya kushindwa kutetea taji lao la Ligi Kuu, LaLiga, Barcelona walikumbana na kichapo kibaya cha mabao 7-1 kutoka kwa Bayern Munich kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na wakamaliza msimu bila taji kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2007-08.

Kama hiyo haitoshi, nahodha wa klabu hiyo, Lionel Messi alionyesha nia ya kutaka kuondoka kabla ya kukubali kubaki, ili kumalizia kipindi chake cha msimu mmoja kilichobaki kwenye mkataba wake.

Koeman alipewa timu hiyo, huku akishuhudia Luis Suarez akiondoka na kwenda kujiunga Atletico Madrid.

Na sasa Barcelona ambayo mashambulizi yake yanaongozwa na Messi na Antoine Griezmann, kiwango chake si cha kuvutia sana kwenye Ligi Kuu, kwani wamepitwa pointi tisa na wapinzani wao wakubwa Real Madrid baada ya mechi saba. Na walifungwa kwenye mchezo wa Clasico.

### #2. Ole Gunnar Solskjaer (Manchester United)

Ole Gunnar Solskaer anaweza kuwa mmoja wa makocha ambao nafasi zao zipo kwenye hatari kubwa msimu huu, kutokana na kiwango kisichovutia cha Manchester United kwenye Ligi Kuu England.

Baada ya kuchezea kichapo cha mabao 6-1 kutoka kwa Tottenham, United na Solskjaer wakapoteza kwa vijana wa Arsenal nyumbani kwenye mchezo wa Ligi Kuu ikiwa ni mara ya kwanza kwa kipindi cha zaidi ya muongo mmoja.

Kiukweli Man United imekuwa ikisuasua kwenye Ligi Kuu kwani haijashinda mchezo wowote kati ya minne ya nyumbani kwenye Ligi Kuu, ikiwa ni mara ya kwanza tangu msimu wa 1972-73, wakati walipomaliza ligi wakiwa nafasi ya 18.

Ulaya, Man United ilishinda mechi mbili za kwanza za Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini ikashindwa kung'ara mbele ya Istanbul Basaksehir. Kacha huyo raia huyo wa Norway kama atashindwa kubadilisha kiwango pale Old Trafford, kuna uwezekano mkubwa wa kutimuliwa kazi hiyo kabla ya msimu huu.

### #1. Zinedine Zidane (Real Madrid)

Linaweza kuwa jambo lisilofikirika kwamba, Zinedine Zidane, ambaye alishinda mataji matatu mfululizo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na mawili ya LaLiga kwa Real Madrid, kukabiliwa na uwezekano wa kufukuzwa msimu huu.

Hata hivyo, inaonekana wazi kwamba, vijana hao wa Zidane hawapo kwenye nafasi nzuri zaidi msimu huu kwenye LaLiga na wanaweza wasilitetee taji hilo.

Ingawa Real Madrid walishinda mchezo wa nyumbani dhidi ya wapinzani wao wakubwa, Barcelona, lakini kiwango chao bado hakijaimarika.

Walifungwa na Cadiz iliyopanda daraja kabla ya kuchezea kichapo cha mabao 4-1 kutoka Valencia pale Mestalla na sasa wamejikuta wakiwa wamepitwa pointi nne na vinara wa ligi hiyo, Real Sociedad baada ya mechi nane. Zidane kama atashindwa kubadilisha kiwango cha timu hiyo, kuna uwezekano mkubwa kibarua chake kikaota nyasi kabla ya mwishoni ma msimu huu.

## ISIKUPITE

APRILI 10, 1973, ndiyo siku aliyozaliwa beki wa zamani wa Real Madrid na Brazil, Roberto Carlos. Ndiye beki aliyefunga mabao mengi zaidi (mabao 16) katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kuliko beki yeyote yule hadi sasa, pia alikuwa mchezaji wa kwanza kutoa pasi mbili za mwisho (assists) kwenye mechi ya fainali ya michuano hiyo katika karne hii ya 21.



Extra Time

# MABEKI 10 WALIOFUNGA MABAO MENGI KARNE 21


RAMOS

**LONDON,** England

JUKUMU muhimu kwa beki kwenye mchezo wa soka ni kuilinda timu yake na mashambulizi, au kwa maneno mengine, kulinda timu pinzani isiwafunge.

**Hata hivyo, walinzi hao pia huingia kwenye kazi ya kuifungia mabao timu yao. Kwa maana nyingine inakuwa kazi ya ziada kwao kwenda kushambulia.**

Mabao ya walinzi hao yanakuwa msaada mkubwa kwa timu pale wanapopanda kusaidia mashambulizi. Makala haya yanakuchambua walinzi 10 bora wanaongoza kwa kufunga mabao, kuna waliostaafu na wengine wanaendelea kucheza, wafahamu sasa...

### #10. ANDREAS HOLZL – MABAO 52

Baada ya kuanza soka la ushindani na klabu ya FC Wacker Innsbruck katika Ligi Daraja la Pili nchini Austria msimu wa 2003-04, Andreas Holzl ametengeneza jina lake na kuwa mmoja wa walinzi wafungaji bora nchini humo.

Mlinzi huyo wa kulia mwenye umri wa miaka 35, amefunga mabao 35 kati ya 52 wakati wa misimu sita akicheza Ligi Daraja la Kwanza katika klabu ya Sturm Graz, huku 12 akifunga katika msimu wake wa kwanza na klabu hiyo.

### #9. MARC DAL HENDE – MABAO 52

Baada ya kuanza kucheza soka katika Klabu ya Vyborg mwaka 2009, Marc Dal Hende amezichezea klabu tano tofauti kwenye Ligi Daraja la Kwanza nchini Denmark.

Mlinzi huyo wa kushoto, Hende amefurahia kipindi chake kikubwa cha uchezaji katika Klabu ya Midtjylland, akifunga mabao 22 katika misimu minne aliyokaa na klabu hiyo.

### #8. PHILIPPE CLEMENT – MABAO 53

Alicheza msimu mmoja tu kwenye Ligi Kuu England akiwa na klabu ya Coventry City, lakini Philippe Clement alitumia misimu 15 katika kipindi chake cha uchezaji akiwa kwenye Ligi Kuu ya Ubelgiji.

Mlinzi huyo wa kati, ambaye alianza kucheza soka la ushindani katika Klabu ya Genk, baadaye akajiunga na Club Brugge, alifunga mabao 50 kati ya 52 kwa klabu hiyo akishinda mataji mawili ya Ligi Kuu ya Ubelgiji.

Clement, ambaye kwa sasa ni kocha wa Club Brugge, alishinda taji la ligi msimu wa 2019-20 akiwa na klabu hiyo.

### #7. DANI ALVES – MABAO 58

Mmoja wa walinzi wa pembeni mwenye uwezo mkubwa wa kufunga katika soka la kisasa, Dani Alves amecheza katika klabu tatu bora tofauti barani Ulaya.

Hata hivyo, ilikuwa pale Barcelona ndiko ambako beki huyo wa kulia alipotengeneza jina lake. Kwa kipindi cha misimu nane yenye mafanikio pale Camp Nou, Alves alifunga mabao 21 na kutoa pasi za mwisho 101.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 raia wa Brazil, ameshinda mataji 20 na klabu hiyo – sita yakiwa ya LaLiga na matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alves baadaye alikwenda kucheza Juventus na Paris St Germain, kabla ya kurudi nyumbani kwake Brazil mwaka 2018, na sasa anacheza pale katika Klabu ya Sao Paulo.

### #6. CHRIS JANSSENS – MABAO 58

Chris Jannsens ni mmoja walinzi wafungaji bora kwenye historia ya Ligi Kuu ya Ubelgiji.

Mlinzi huyo wa kati amefunga jumla ya mabao 58 baada ya kuanza kucheza soka la ushindani katika Klabu ya KSC Lokeren kwenye Ligi Kuu Ubelgiji.

Jannsens amefunga nusu ya mabao yake - 26 – wakati akicheza pale KVC Westerlo. Katika msimu wa 2000-01, Jannsens alifunga mabao 12 kwa KSC Lokeren baada ya kufunga 12 kwa klabu hiyo msimu mmoja kabla.

### #5. WILLIAM JANSSEN – MABAO 59

William Janssen amefunga mabao ya kuvutia 59 tangu alipoanza kucheza soka la ushindani katika Klabu ya VVV Venlo ya Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, msimu wa 2006-07.

Mlinzi huyo wa kati mwenye umri wa miaka 34, amefunga mabao 24 kwa klabu yake ya sasa ya Utrecht, ambayo alijiunga nayo mwaka 2013.

Jannsen pia amefunga mabao 20 kwa Roda na 13 kwa Twente, ambako alishinda taji la Super mwaka 2012. Msimu uliopita, Janssen alikuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao 13 mfululizo kwenye Ligi Kuu Uholanzi kwa karne hii.

### #4. ROBERTO CARLOS – MABAO 65

Mmoja wa walinzi bora zaidi wa kushoto wa wakati wote, Roberto Carlos ambaye aling'ara kwa uwezo wake wa kufunga akiwa na klabu za Inter Milan na Real Madrid.

Carlos, anatambulika kwa uwezo wake wa kufunga mabao ya adhabu ndogo kwa mashuti makali.

Nyota huyo wa zamani wa Brazil, alifunga bao kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, katika kila msimu kwa misimu 11 aliyocheza pale Real Madrid na kutoa pasi za mwisho katika misimu yote kasoro miwili. Akiwa kwenye kiwango chake bora kabisa kwenye miaka ya 2000, mlinzi huyo wa kushoto alifunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho wakati Real Madrid ikishinda taji la LaLiga mwaka 2000 na 2002.

### #3. JAMES TAVERNIER – MABAO 67

Baada ya kuanza kucheza soka la ushindani katika Klabu ya Newcastle United mwaka 2009, James Tavernier amejijengea jina lake mwenyewe kwa kuwa beki mwenye uwezo mkubwa zaidi wa kufunga mabao kwa miamba ya soka la Scotland, klabu ya Rangers.

Kwa kipindi cha muongo mmoja wa kucheza soka, beki huyo mwenye umri wa miaka 29, amefunga mabao 67 na kutoa pasi za mwisho 96 katika mashindano yote.

### #2. RENE AUFHAUSER – MABAO 71

Rene Aufhauser ni mmoja wa walinzi wafungaji bora kabisa katika karne hii. Kwa kipindi cha miongo miwili ya kucheza soka la kulipwa, mlinzi huyo wa kati wa Austria alicheza mechi 100 kwa klabu tatu tofauti - Austria Salzburg, Grazer AK na Red Bull Salzburg.

Hata hivyo, mlizi huyo wa kati mwenye umri wa miaka 44, ambaye alikuwa na uwezo mkubwa wa kucheza nafasi ya kiungo wa kati, alipata mafanikio makubwa zaidi akiwa na Red Bull Salzburg, akishinda mataji matatu ya Ligi Kuu ya Austria na kufunga mabao 50.

### #1. SERGIO RAMOS – MABAO 103

Sergio Ramos ni mmoja wa walinzi wa kati bora zaidi wenye uwezo mkubwa wa kufunga mabao katika karne hii.

Nahodha huyo wa Real Madrid aliiongoza klabu yake hiyo msimu uliopita kutwaa taji lao la kwanza la Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, kwa kipindi cha miaka mitatu.

Tangu kuondoka kwa mfungaji aliyeweka rekodi katika klabu hiyo, Cristiano Ronaldo, Ramos pia ndiye kama amechukua majukumu ya kufunga mabao kwa sasa.

Mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 34, alipiku rekodi ya Ronald Koeman ya kuwa beki aliyefunga mabao mengi (67) kwenye historia ya LaLiga.

Mapema mwezi huu, Ramos alifunga bao lake la 100 kwa Real Madrid na kuungana na Fernando Hierro kuwa mlinzi pekee karne hii kufunga mabao mengi kwa miamba hao wa soka la Hispania.

## Nukuu

"Watu wanasema ni nani mchezaji bora duniani? Na wengi wanasema kwa usahihi Messi, huwezi kupinga maoni hayo. Lakini Ronaldo anaweza kuichezea Millwall, Queens Park Rangers, Doncaster Rovers... klabu yoyote, na kufunga hat-trick katika mchezo huo. Sina uhakika kama Messi anaweza kulifanya hilo. Ronaldo ana miguu miwili, ni mwepesi, mzuri hewani, mkakamavu – Messi ni mkakamavu bila shaka. Nadhani Messi ni mchezaji wa Barcelona zaidi," **Kocha wa zamani wa Manchester United, Sir Alex Ferguson, akizungumzia mjadala wa nani bora kati ya Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.**



"Kikatiba, Neymar hayupo kwenye mipango yangu, kwa sababu ya kifedha na nyinginezo, kama kesi aliyofungua ya madai dhidi ya klabu na ukweli kwamba aliondoka klabuni kwa hali ambayo si nzuri kabla ya kuanza kwa msimu mwaka 2017," **Mgombea urais wa Barcelona, Victor Font, ambaye awali alibainisha mpango wa kutaka kumrudisha Pep Guardiola pale Catalunya kuungana na Lionel Messi.**




"Bado ninajaribu kujifua ili kuendelea kuwa katika mwonekano mzuri, lakini katika mazoezi ya vipindi vya mara kwa mara gym. Sikosi mazoezi hata kidogo, kwa uhakika, Cristiano [Ronaldo] ni mwenye kasi zaidi yangu. Kwangu mimi, anafanya kazi kila siku, yeye ni mwanariadha bora. Mara zote yupo kileleni mwa mchezo, hakika nadhani atakuwa na kasi zaidi yangu kwa sasa," **Mshindi wa zamani wa mbio za olimpiki za mita 100, Usain Bolt.**





Wachezaji wa Simba wakishangilia moja ya mabao saba waliyoifunga Coastal Union kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, iliyopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# COASTAL INAVYOGEUZWA SHAMBA LA MABAO BARA

**Na Adam Fungamwango**

COASTAL Union ya Tanga, imekutana na kipigo kikali cha mabao 7-0 kutoka kwa Simba Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

**Hii si mara ya kwanza kwa timu hiyo kushindiliwa idadi kubwa ya mabao na Simba kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara. Msimu wa 2018/19, ilikubali kipigo cha mabao 8-1.**

Kwenye mechi hiyo, Hassan Dilunga na Clatous Chama ambao walifunga mabao msimu wa 2018/19, Jumamosi iliyopita wamerudia tena kuwa sehemu ya 'wauaji' wa Coastal Union kwa mara nyingine tena msimu huu.

Mechi zote mbili za msimu wa 2018/19 na ya Jumamosi, zimezalisha 'hat-trick' tatu, mbili za misimu miwili iliyopita na moja ya msimu huu.

Rekodi zinaonyesha kuwa Coastal Union imekuwa ikipokea kipigo cha mabao mengi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kila baada ya misimu kadhaa. Tangu mwaka 2011, hadi 2020, Coastal imeshakutana na vipigo sita vitakatifu kutoka timu mbalimbali.

Katika makala haya yamekusanya mechi zote ambazo Coastal ilikutana na dhahama ya vipigo vizito kwenye Ligi Kuu Bara, twende sasa...

**#1. Coastal 0-5 Yanga (2011/12)**

Rekodi mbaya ya Coastal Union kupokea vipigo vikubwa ilianza Septemba 28, 2011, ikiwa ni msimu wa 2011/12, ikicheza dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Taifa kwa sasa ukitwa Benjamin Mkapa.

Coastal ilikubali kipigo cha mabao 5-0. Mabao ya washindi yalifungwa na straika Mghana Kenneth Asamoah, akipachika mabao mawili kwenye mechi hiyo, Shamte Ally, akifunga moja, straika Mzambia Davis Mwape akifunga bao moja na Nurdin Bakari akihitimisha hesabu.

**#2. Coastal 0-4 Azam FC (2013/14)**

Ilikuwa ni Machi 15, 2014 kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara katika Uwanja wa Azam Complex, Coastal ilipokubali kipigo kingine cha mabao 4-0, ikiwa ni ligi ya msimu 2013/14 dhidi ya Azam FC.

Mabao ya Azam, yaliwekwa wavuni na winga machachari wa timu hiyo wakati huo raia wa Ivory Coast, Kipre Tchetche akipachika mawili, John Bocco ambaye kwa sasa yupo Simba na Kelvin Friday kila mmoja akichungulia nyavu mara moja.

**#3. Coastal 0-8 Yanga (2014/15)**

Kipigo kingine cha fedheha ilikipata Coastal Union kwenye Uwanja wa Taifa ambao sasa unaitwa Benjamin Mkapa ilikuwa Aprili 8, 2015, ikiwa ni msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2014/15. Ilikutana na kisago cha mabao 8-0 kutoka kwa Yanga.

Ni mechi iliyozalisha 'hat-trick' kama ile ya Jumamosi iliyopita kupitia kwa John Bocco. Hii ilikuwa ni kwa straika Mrundi Amissi Tambwe, ambaye kwenye mechi hiyo alifunga mabao manne peke yake. Mabao mengine yalifungwa na winga wa kimataifa ambaye kwa sasa amesajiliwa na Wydad Casablanca ya Morocco, Simon Msuva aliyefunga mawili, Kpah Sherman straika raia wa Liberia, na Salum Telela akikamilisha kipigo hicho.

**#4. Coastal 0-4 Mbeya City (2015/16)**

Ikiwa katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya Aprili 2, 2016, kwenye Ligi Kuu msimu wa 2015/16, Coastal ilichabangwa mabao 4-0 na kuendelea na rekodi yake mbovu ya kuwa timu inayofungwa idadi kubwa ya mabao mara kwa mara kila msimu wa ligi.

Mabao ya Mbeya City yaliwekwa wavuni na Salvatory Nkurula aliyefunga mawili, Hassan Mwasapili na Ditram Nchimbi ambaye kwa sasa anaichezea Yanga naye akiingia kambani.

**#5. Coastal 1-8 Simba (2018/19)**

Ilikuwa ni Jumatano ya Mei 8, 2019, msimu wa 2018/19, Coastal ilipokubali kufungwa mabao 8-1 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.


Zilikuwa ni 'hat-trick' mbili za mastraika wa kimataifa wa Uganda, Emmanuel Okwi na Mnyarwanda, Meddie Kagere, zikizaa mabao sita, huku Hassan Dilunga na Clatous Chama wakifunga bao moja kila mmoja, wakati Raizin Hafidh akiifungia timu yake bao pekee la kufutia machozi.

**#6. Coastal 0-7 Simba (2020/21)**

Hii ndiyo mechi iliyochezwa Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba ikiinyanyambua Coastal mabao 7-0.

Dilunga ambaye alifunga kwenye mechi ya msimu 2018/19, alifunga bao la kwanza juzi, Bocco akifunga 'hat-trick', na Chama ambaye alifunga kwenye mechi ya msimu wa 2018/18, akiifunga tena Coastal Union, safari hii akipachika mawili mguuni mwake.

**JE, WAJUA?**



100 - ni mabao aliyofunga beki wa kati wa Real Madrid na Hispania, Sergio Ramos hadi sasa katika mashindano yote, kati ya hayo, 55 amefunga kwa kichwa.



# Sababu ajira za watoto zaanikwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa hali duni ya maisha kwa baadhi ya wazazi na walezi ni chanzo cha watoto wengi kuingia kwenye mfumo wa ajira zisizo rasmi wakiwa na umri mdogo ikiwamo kufanya kazi za ndani.

Ofisa Habari na Mawasiliano kutoka Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF), Celina Baragwiha, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na Nipashe jijini hapa kuhusu Siku ya Kimataifa ya Watoto.

Alisema hali hiyo inasababisha kuzima kwa ndoto zao na kuathiriwa na ukatili wa kisaikolojia kwa kuwa watoto wengi wanatumikishwa bila kupata ujira.

"Kwa mfano tulizungumza na wazazi katika Kata ya Lubeta, baadhi yao wanasema tunapeleka watoto wetu Dar es Salaam kwa sababu ya umaskini, halafu wakifika kule mshahara atakaolipwa unakwenda kwa mzazi," alisema.

Alisema wazazi wapo kwenye sehemu ya utumikishaji watoto kutokana na wao kupokea mshahara badala ya mtoto anayefanya kazi.

Ofisa huyo alisema licha ya elimu inayotolewa ya kutetea haki za watoto na wadau wakiwamo CDF bado jamii imekuwa ikipuuza na kuendelea kutumikisha watoto.

"Hata kama wanapatiwa elimu bado wanaendelea kufanya na mtu hajaamua kubadilika kwa sababu tu ya mazoea, ukisikiliza waliofanyiwa ukatili unaona kabisa sio kitu cha ubinadamu, kuna watu wanaona watoto hawa sio binadamu, hawa nao wana haki zao tuzingatie," alisema.

Akizungumzia hali ya utumikishwaji wa mtoto hususan wa kike katika Mkoa wa Lindi, Mkuu wa Idara ya Usimamizi na Tathmini na Mafunzo kutoka Asasi ya Vijana ya TYVA, Peter Masoi, alisema mtoto wa kike amekuwa akichukuliwa kama sehemu ya kupunguza majukumu ya familia na hivyo kumnyima haki zake za msingi.

"Kwa mfano wa Lindi bado hakuna ufahamu mkubwa wa haki za binti haujaifikia jamii, kule mtoto wa kike amekuwa akichukuliwa kama sehemu ya kupunguza majukumu ya familia, wanatumikishwa ndio maana wanajikuta wakijiingiza kwenye ndoa wakiwa na umri mdogo au kukimbia nyumbani," alisema.



Mkulima wa mtama katika eneo la Kibaigwa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, Sebastian Msola (kulia), akitoa maelezo kwa ujumbe kutoka TBL , WFP na FtMA walipofika kumtembelea shambani kwake mwishoni mwa wiki, wakati wa tathmini ya mradi wa pamoja wa kuwezesha wakulima wa zao hilo katika mikoa ya Dodoma na Manyara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge aahidi visima vingine

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, ameahidi kuchimba visima vingine 20 ndani ya Jiji la Dodoma ili kutatua kero ya maji.

Akizungumza jana wakati akizindua kisima cha maji katika eneo la Chikola, Kata ya Matumbulu kilichochimbwa kwa ufadhili wa Taasisi ya Islamic Help Tanzania kwa ushirikiano na Taasisi ya DABBAGH Welfare Trust ya Denmark, Mavunde alisema kuna maeneo bado hayana huduma ya majisafi na salama hivyo atahakikisha yanapata huduma hiyo.

"Mmekuwa mkitembea umbali mrefu sana kufuata maji, kilometa kwa kilometa, imesababisha kutumia muda mwingi kutafuta maji na kushindwa kufanya shughuli nyingine, leo nina furaha kubwa kwamba ndoto yetu ya kupata maji imekamilika," alisema.

Alisema utekelezaji huo ni moja ya ahadi alizotoa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu mwaka huu, ambapo aliahidi kutatua tatizo la maji kwa wananchi.

"Nataka ndani ya muda mfupi sana tuondoe tatizo la maji kata nzima ya Matumbulu. Niliangalia namna ya kutafuta wadau kusaidia hili nashukuru Mungu hawa wadau wamekubali kunisaidia kutatua tatizo la maji," alisema.

Alifafanua kuwa kisima hicho alichozindua kitanufaisha kaya 370 na wananchi zaidi ya 2000, ambapo awali walikuwa wanatembea zaidi ya kilometa nne kufuata maji.

Alisema pia Taasisi ya Islamic Help imeahidi kusaidia wananchi wenye mifugo ili kukuza uchumi wao.

Kwa upande wake Mwakilishi wa taasisi hiyo, Ahmed Munir, alisema ipo tayari kushirikiana na wakazi wa Dodoma Mjini kupitia ofisi ya mbunge kutatua kero ya maji kwa wananchi.

"Kwa sasa tumekuja kuangalia maeneo mengi zaidi yanayohitaji huduma ya maji kwa ajili ya kuanza utekelezaji mkubwa wa uchimbaji wa visima kwenye jimbo hili," alisema.

Wakizungumza baada ya kuzinduliwa kwa mradi huo wa maji Matumbulu, wananchi walimshukuru mbunge kwa jitihada zake za kutatua kero zinazowakabili.

Mmoja wa wananchi hao, Janeth Matonya, alisema walikuwa wakichota maji kwenye visima vya kienyeji vilivyochimbwa jirani na bwawa lililopo Matumbulu.

"Ni muda mrefu hakuna maji mimi nimezaliwa nimekuta hii kero, kwa kweli tunamshukuru mbunge wetu Mavunde kwa kutuletea maji na wafadhili tumepata maji salama sasa," alisema.

Kwa upande wake, Josia Masebo, alisema wananchi walikuwa wanachota maji yanayotumiwa na mifugo, lakini kwa sasa afya zao zitaimarika kutokana na kupata maji safi na salama.

## Baraza la Wafanyakazi Wizara Mambo ya Ndani lashauriwa

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

BARAZA la Wafanyakazi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, limetakiwa kujenga utaratibu wa kukutana na menejimenti ya wizara ili kuishauri namna ya kuweka mikakati bora ya ufanyaji kazi kwa watumishi.

Katibu Mkuu Wizara hiyo, Christopher Kadio, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akifungua mkutano wa baraza hilo uliofanyika jijini hapa.

Alisema hatua hiyo itasaidia kukumbushana majukumu kwa kila mmoja wao.

Aidha, aliwataka watumishi wa wizara hiyo kutatua kero za wananchi kwa wakati zinapowasilishwa kwenye vitengo vyao vya kazi.

Alisema kuna kila sababu ya kufanya tathmini ya utendaji wa kazi wa kila mmoja katika kitengo chake ili kuboresha mazingira ya kazi.

"Naomba nyie mliokuja kuwawakilisha wenzenu mkawe mfano wa kuigwa katika sehemu zenu za kazi, lakini mkawape elimu wenzenu waliowachagua kuja kuwawakilisha katika mkutano huu wa baraza, ili nao wasibaki nyuma kiutendaji," alisema Katibu Mkuu huyo.

Kadio alisema wakizingatia hilo, baraza hilo litasaidia watendaji wa wizara kuwajibika kwa weledi katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Alisema baraza hilo ni jukwaa la kisheria la majadiliano ya pamoja ya namna ya kuboresha ufanisi wa kazi.

Aliwataka kutumia nafasi hiyo vizuri kuhakikisha wanapanga mikakati ambayo italeta tija kwa wizara na kwa taifa kwa ujumla.

Naye Mwenyekiti wa Baraza hilo, Emmanuel Kayuni, alisema baraza litatenda haki kwa kujadili masuala ya yanayohusu haki na maslahi ya wafanyakazi.

Alisema wajumbe wa baraza hilo watatekeleza waliyoagizwa na litakuwa mfano wa kuigwa na mabaraza mengine kutokana na utendaji wake.

"Nikuhakikishie Katibu Mkuu sisi tupo hapa kwa ajili ya wenzetu, hivyo kile tunachojadili tutakifikisha kwa wenzetu na kufanyia kazi," alisema Kayuni.





## Wafugaji waomba kujengewa josho

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAFUGAJI wa Kata ya Mjere katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuwajengea josho kwa ajili ya kuogesha mifugo yao kwa maelezo kuwa kwa sasa wanatembea umbali mrefu kwenda kuogesha kwenye majosho yaliyoko katika Wilaya ya Songwe.

Wakizungumza na Nipashe juzi, baadhi ya wafugaji hao walisema mifugo yao imekuwa ikishambuliwa na magonjwa pamoja na wadudu kutokana na baadhi ya wafugaji hao kushindwa kwenda katika kata za jirani.

Mmoja wa wafugaji hao, Jangson Mwotela, alisema baadhi ya wafugaji wamekuwa wakitumia mbinu za kienyeki kuogesha mifugo yao kwa kupulizia dawa mbinu ambayo inahitaji umakini mkubwa ili kutoidhuru mifugo.

"Hapa tuna mifugo mingi sana lakini tatizo letu ni kushindwa kuiogesha kwa sababu hatuna majosho yaliyopo jirani, sasa tunaiomba serikali itusaidie kujenga majosho ili nasi tuboreshe mifugo yetu," alisema Mwotela.

Naye Mbozyo Shila, alisema kutokana na uhitaji walionao wa majosho wako tayari kushirikiana na serikali kujenga majosho hayo kwa kuchangia michango yao ya hali na mali ili kuyakamilisha.

Mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa wadau wa kilimo na mifugo wa kujadili rasimu ya kilimo ya miaka mitano, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya Uchumi na Uzalishaji, Said Madito, alisema mkoa huo una zaidi ya mifugo milioni 3.3.

# Sababu kuongezeka magonjwa yasiyoambukiza

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IMEELEZWA kuwa magonjwa yasiyoambukiza yanaongezeka kwa kasi nchini kutokana na mabadiliko ya mfumo wa maisha, likiwamo ongezeko la watu kuacha kutembea kwa miguu na badala yake wanatumia vyombo vya moto.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia maadili ya Tafiti za Afya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Dk. Godlove Mbwanji, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa maadhimisho ya miaka 40 ya kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu nchini (NIMRI).

Alisema miaka ya nyumba magonjwa yasiyoambukizwa yakiwamo magonjwa ya moyo, kisukari na shinikizo la damu yalikuwa yanawakabili matajiri kutokana na mifumo yao ya maisha, lakini kwa sasa hata watu wenye kipato cha kawaida wanaugua.

Alisema sababu kubwa ni ongezeko la matumizi ya vyombo vya moto ikiwamo pikipiki za kubeba abiria (bodaboda), pikipiki za magurudumu matatu (bajaji) na magari ya abiria hali inayowafanya watu wengu kuacha kutembea kwa miguu.

"Zamani tulikuwa tunaamini magonjwa haya ni ya matajiri kwa sababu wao ndio walikuwa na uwezo wa kula vyakula vya mafuta na kutembelea magari kila muda, lakini sasa hivi kuna vibajaji na pikipiki ambazo kila mmoja anapanda na hakuna anayefanya tena mazoezi," alisema Dk. Mbwanji.

Akifungua maadhimisho hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alishauri Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kuongeza ubunifu wakati wa ujenzi wa barabara kwa kuweka maeneo ambayo watu watakuwa wanafanyia mazoezi ya viungo.

Chalamila alisema maeneo hayo yakianzishwa, watu wengi watahamasika kufanya mazoezi ambayo yatawasaidia kuepuka magonjwa yasiyoambukizwa ambayo kwa sasa yamekuwa tishio kutokana na watu kutofanya mazoezi.

"Badala ya ku-invest (kuwekeze) mabilioni ya fedha kwenye matibabu ya magonjwa haya yasiyoambukiza, ni vema sasa tukawekeza fedha hizo kwenye maboresho ya barabara zetu," alisema Chalamila.

Aliwataka wananchi kubadili mfumo wa maisha kwa kuanza kufanya mazoezi, ili kukabiliana na magonjwa hayo ambayo hata matibabu yake ni magumu na ni gharama kubwa kuliko kuyaepuka.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa NIMRI, Dk. Ndekya Urio, alisema kwa sasa taasisi hiyo inafanya utafiti zaidi ya 120 ukiwamo wa magonjwa yasiyoambukiza kama kisukari na shinikizo la damu.

Alisema taasisi hiyo itakuwa inatoa taarifa za matokeo ya kila utafiti kama walivyokuwa wanafanya kwenye magonjwa mengine yanayoambukizwa.

Naye Mkurugenzi wa NIMRI Kituo cha Mbeya, Dk. Nyanda Julius, alisema kituo hicho kina maabara kubwa na yenye vifaa vya kutosha kwa ajili ya kufanikisha kila aina ya utafiti wanaofanya huku akidai kuwa maabara hiyo imekuwa ya mfano nchini.

Alisema wanafunzi kutoka katika taasisi mbalimbali za elimu za ndani na nje ya nchi wamekuwa wakienda kujifunza na kufanya mazoezi ya utafiti kwenye kituo hicho.




Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, akizungumza na wananchi kutoka mikoa tisa ambao wamehudhuria kongamano la sita la jinsia ngazi ya wilaya, ambalo limehitimishwa juzi, Kijiji cha Hatwelo, Kata ya Ijombe Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya. Moja ya mambo aliyoyatilia mkazo ni wanaume wa mkoani Mbeya kuacha tabia ya kupenda kulelewa na wake zao na kuwaachia jukumu la kutunza na kuhudumia familia. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mkoa wa Mbeya kuongeza usambazaji mbolea

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya unakusudia kuongeza usambazaji wa mbolea kwa wakulima kutoka tani 88,909.9 mwaka huu, mpaka tani 115,582.87 katika kipindi cha miaka mitano ijayo, ili kuongeza uzalishaji na tija kwenye kilimo.

Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Mbeya, Said Madito, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa wadau wa kilimo na mifugo wa kujadili rasimu ya mpango mkakati wa kilimo ya miaka mitano kuanzia mwaka 2021 mpaka 2025.

Alisema pamoja na ongezeko hilo la mbolea pia wanatarajia kuongeza usambazaji wa mbegu bora za mazao mbalimbali kutoka tani 72,176.3 mpaka tani 79,393.93 katika kipindi hicho, huku akisisitiza kuwa pembejeo hizo zitakuwa zinapatikana kwa bei nafuu.

Madito alisema vilevile wanakusudia kuongeza usambazaji wa viuatilifu mbalimbali vikiwamo yabisi na vimiminika kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kukabiliana na wadudu waharibifu wa mazao pamoja na magonjwa yanayoshambulia mazao yao.

"Lengo letu ni kuwasaidia wakulima kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao yao, lakini tutahakikisha maofisa ugani wetu wanafanya kazi kwa nguvu wakishirikiana na viongozi wengine wa serikali kuhamasisha wananchi kulima," alisema Madito.

Vilevile alisema ili kuongeza upatikanaji wa mbolea mkoani humo, Serikali ya Mkoa inaendelea kuhamasisha wadau kuanzisha kiwanda kimoja cha kuzalisha bidhaa hiyo ifikapo mwaka 2025.

Pia alisema serikali inakusudia kuboresha vituo 10 vya rasilimali za kilimo vya kata kwa kuviwekea teknolojia za kisasa, ili kuwasaidia wadau kupata taarifa mbalimbali kwa njia ya kielektroniki.

Baadhi ya wadau wa kilimo waliohudhuria mkutano huo waliiomba serikali kutafuta masoko ya uhakika kwa ajili ya mazao ya wakulima, ili wakulima wanapohamasishwa kulima wawe na uhakika wa soko.

Mmoja wa wadau hao, Bakari Juma, ambaye ni Meneja wa Chama Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku wilayani Chunya (CHUTCU) alisema wakulima wengi huwa wanakosa hamasa ya kuzalisha zaidi mazao kutokana na kukosa uhakika wa soko.

Alisema wakati mwingine wakulima wanatumia nguvu na gharama kubwa kwenye uzalishaji wa mazao, lakini bei za wanunuzi zinawakatisha tamaa wakulima.

"Tunaomba sana wakati tunaendelea kuhamasisha wakulima kuzalisha tunatakiwa tuwahakikishie na soko la mazao hayo na soko lenyewe liwe ni lenye tija," alisema Juma.

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, alisema wakati wa maboresho ya mpango mkakati huo wanatakiwa wazingatie Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka huu.

Alisema vipaumbele vya kilimo katika miaka mitano ijayo ni muhimu kwa sababu sasa hivi serikali inatekeleza sera ya uchumi wa viwanda ambao unategemea zaidi kilimo kwenye uzalishaji wa malighafi.



# 26,600 kufanya mtihani kidato cha 4

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohamed Said, amesema mitihani ya kidato cha nne inatarajiwa kuanza kesho, jumla ya wanafunzi 23,621 wanatarajiwa kufanya mitihani hiyo kwa Zanzibar, huku wakionywa kufanya udanganyifu.

Akitoa taarifa ya mitihani kwa waandishi wa habari, Simai amesema miongoni mwa watahaniwa hao 14,061 sawa na asilimia 59.3 ni wanawake na watahiniwa 9,605, sawa na asilimia 40.7 ni wanaume.

Alisema kuna jumla ya vituo 232 vya kufanyia mtihani wa elimu ya lazima kidato cha nne kati ya hivyo vituo 172 ni vya shule za serikali na vituo 60 shule binafsi.

Aliwataka wanafunzi kuachana na vitendo vinavyoashiria udanganyifu wakati wote wa mitihani yao na vinaweza kusababisha kuharibia matokeo yao.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idrissa Muslim Hija, alisema ili watahaniwa wote wapate matokeo ya daraja la kwanza ni vyema kuwa watulivu na kufuata maelekezo kwa makini ili kufikia malengo yao.

Kwa upande wake, Ofisa Mdhamini Wizara hiyo Pemba, Mohammed Salim Nassor, alisema maandalizi ya mitihani kwa upande wa Pemba yamekamilika na kuiomba jamii kuwapa ushirikiano wa hali ya juu watahiniwa ili kufikia malengo yao na kuiletea sifa taifa ya ufaulu mzuri.

Mkurugenzi wa Idara ya Elimu Sekondari, Asya Iddi Issa, alisema wizara kwa kushirikiana na maofisa elimu wa mikoa yote Zanzibar imejipanga vyema kuhakikisha mazingira, miundombinu na vifaa vyote vya shule mbalimbali vinakuwa katika mazingira mazuri na salama ili kuwawezesha wanafunzi kufanya mitihani yao kwa utulivu.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Suraga, akizungumza na wafanyakazi wa Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) baada ya kula kiapo juzi, Ikulu Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mawaziri waahidi kufanya makubwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAWAZIRI wa serikali ya Zanzibar, wameahidi kutekeleza kwa vitendo Ilani ya uchaguzi wa CCM, ahadi zilizotolewa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi wakati wa kampeni pamoja na maelekezo yaliomo katika hotuba aliyoitoa katika ufunguzi wa Baraza la Wawakilishi Novemba 11, mwaka huu.

Wakizungumza na waandishi wa habari juzi, baada ya hafla ya kuapishwa Ikulu Zanzibar, mawaziri hao walisema wataweka mikakati imara na kuwa wabunifu katika usimamizi wa majukumu hayo, ili kuimarisha uchumi na kuwandolea kero wananchi, hususan katika suala la upatikanaji wa huduma.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema ataendeleza juhudi zilizoanzishwa katika serikali ya awamu ya saba ili kufanikisha mapambano dhidi ya rushwa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Jamal Kassim Ali, alisema ataweka mikakati mizuri katika ukusanyaji wa mapato pamoja na kusimamia matumizi mazuri ya fedha za serikali.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema atahakikisha fedha za mfuko wa maendeleo ya jimbo zinatumika vyema na kwa utaratibu uliowekwa ili ziweze kuleta tija katika maendeleo ya wananchi.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohamed Said, alieleza kuwa atatumia uwezo wote pamoja na ubunifu katika kukabiliana na changamoto mbalimbali ndani ya sekta hiyo, ikiwamo uhaba wa madarasa ya kusomea pamoja na kuwataka wazazi na walezi kusimamia maendeleo ya elimu ya watoto wao.

Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohamed, alisema huu ni wakati mwafaka kwa vikosi vya Serikali ya Zanzibar kufanya kazi zaidi za uzalishaji mali, akibainisha kuwapo kwa ardhi ya kutosha itakayoweza kufanikisha azma hiyo.

Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Riziki Pembe Juma, akabainisha namna wizara hiyo itakavyoandaa mikakati madhubuti katika kuliendeleza eneo la ardhi lililoko Bagamoyo Mkoa wa Pwani, linalomilikiwa na Serikali ya Zanzibar.

"Nitasimamia mikakati katika kuimarisha sekta ya utalii kisiwani Pemba kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya utalii, kama kilivyoainishwa katika dira ya 2020-2050", alisema Lela Mohamed Mussa, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale.

## Kaya maskini 16,200 zanufaika ruzuku TASAF

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMLA ya kaya 16,239 zitanufaika na ruzuku ya fedha ya Sh. bilioni 6.8 katika mpango wa kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) awamu ya tatu kwa kanda ya Unguja.

Akitoa taarifa katika kikao cha uidhinishaji wa fedha za mpango huo kwa wajumbe wa kamati ya TASAF Kanda ya Unguja katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mjini Vuga, Mratibu wa TASAF Unguja, Makame Ali Haji, alisema kaya hizo kati ya 17,909 zimekidhi vigezo katika shehia zote 126 za Unguja zinazotekeleza mpango huo.

Alisema lengo la mpango huo ni kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya, pia kuongeza uwezo wa walengwa wa mpango huo, kuhusu uwekaji akiba kwa matumizi na mahitaji ya baadaye pamoja kuwekeza katika miradi ya uzalishaji kwa ukuaji wa uchumi.

"Mpango huu wa kunusuru kaya maskini ni kuziwezesha kaya kuongeza kipato na fursa wakati zikiimarisha matumizi ya kaya hizo, ili ziweze kuishi maisha ya kawaida yatakayowawezesha kupata mahitaji yote ya msingi," alisema Makame.

Aidha, Makame alisema kabla ya kupatiwa fedha kaya hizo zimepatiwa mafunzo ya msingi ya uzalishaji pamoja na uibuaji wa miradi ya walengwa sambamba na kufanyiwa uhakiki.

Kwa upande wao wajumbe wa kamati ya TASAF Unguja wakiongozwa na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Hassan Khatib Hassan, waliushauri mpango huo uzinduliwe kitaifa ili kutambulika zaidi na wananchi katika kunufaika na miradi yao ya ndani.

"Tunashauri kwa vile fedha hizi ni nyingi zinatarajiwa kuwanufaisha watu wetu, mpango huu uzinduliwe kitaifa kwa kuwaomba viongozi wetu wakuu wa nchi ikiwa Rais au Makamu atuzindulie ili wananchi wetu waone matunda ya serikali yao ya awamu ya nane," alisema Khatib Hassan Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.

Zaidi ya Sh. bilioni 6,806,267,150 zitatumika katika mpango wa kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya maskini kupitia TASAF awamu ya tatu kwa shehia 126 za mikoa ya Unguja.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:
- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam - 0768 928 516.**
**Arusha - 0677 226 960.**

## NAFASI ZA MASOMO

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** ILIYOPO SALASALA RTD INATANGAZA NAFASI ZA AWALI NA MSINGI. KWA MAWASILIANO **PIGA SIMU: 0713 327613.**

## NYUMBA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba inauzwa ni ya ghorofa moja, ina frem tatu za biashara zote zina wapangaji. Bei maelewano, ipo Ukonga Dar es salaam. Piga simu namba **0757 079 057.**


*NIPASHE NI JIBU LAKO*
**NJOO UTANGAZE NASI**
**KWA BEI NAFUU SANA**
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA VYETI



116009502

**JOHN MUSSA ELEPHANT** anatangaza kupotelewa na leaving **certificate pamoja na result slip** ya kidato cha sita yenye **index number S0144/0569** iliyotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia Msumba Sekondari mwaka 2020. Yeyote atakayeviokota au kuviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **MWA/NY/RB/813418/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



116009702

**PELICIA PETRO MUSIGULA** anatangaza kupotea na cheti cha **MEDICAL DEGREE CERTIFICATE** chenye namba **K 23 0093** kilichotolewa na **KILIMANJARO CHRISTIAN MEDICAL UNIVERSITY COLLEGE (KCMUCO)** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **KIL/MOS/RB/812980/2020.**

## TAARIFA YA KUFUNGA BEFAO & CO (BFC) LTD

Tunapenda kuutarifu Umma kuwa katika kikao cha Bodi ya Wakurugenzi kilichofanyika tarehe 15/04/2020 kiliazimia kufunga Kampuni ya **Befao & Co (BFC) Ltd** yenye Usajili. No. 135061 kuanzia tarehe **20/04/ 2020.** Kwa maelezo/madai wasiliana na Tel. **0715-388297/0754-388297 au befao2017@gmail.com**


***Uza,***
***Chenye Thamani Kubwa***
***Kwa Kutangaza Nasi Kwa***
***Bei Poa***
***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Makao makuu ya bunge Guatemala yachomwa moto

**GUATEMALA CITY,** Guatemala

MAELFU ya watu wameandamana na kukusanyika kwa amani katika eneo kuu la Jiji la Guatemala, mji mkuu, Novemba 21, mwaka huu, wakipinga kupunguzwa kwa bajeti, hatua iliyochukuliwa na serikali.

Kando na maandamano hayo, waandamanaji wengine wenye hasira walichoma moto makao makuu ya Bunge la nchi hiyo.

Waandamanaji hao walikuwa wamebebelea bendera za nchi hiyo na mabango yaliyoandikwa "Giammattei, ajiuzulu".

Waandamanaji hao walitoa wito kwa Rais Alejandro Giammattei, kupinga bajeti hiyo, iliyopitishwa Jumatano ya wiki iliyopita.

Hali ya sintofahamu inaendelea kuripotiwa katika miji mbalimbali ya Guatemala. **RFI**

## Burkina Faso wapiga kura

**OUAGADOUGOU,** Burkina Faso

WANANCHI wa Burkina Faso walipiga kura jana, kumchaguwa rais mpya na wabunge.

Wagombea 13, ikiwa ni pamoja na rais anayemaliza muda wake, Roch Marc Christina Kabore na mwanamke mmoja watashiriki katika kinyang'anyiro hicho cha urais.

Wakati huo huo Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, ameipongeza serikali, viongozi wa kisiasa na raia wa Burkina Faso kwa kudumisha mazingira ya kuheshimiana katika wakati wote wa mchakato wa uchaguzi, licha ya changamoto lukuki zinazolikabili taifa hilo la Afrika Magharibi.

Katika ujumbe uliotolewa na msemaji wake mjini New York, Marekani, Guterres alitoa wito huo jana kwa wadau wote katika uchaguzi huo kuendeleza mazingira hayo na kuhakikisha kwamba uchaguzi unafanyika kwa njia ya amani, jumuishi na wa kuaminika.

Katibu Mkuu pia alivitaka vikosi vya ulinzi vya nchi hiyo, kufanya kila juhudi kuwalinda raia nchi nzima wakati wakipiga kura kutekeleza haki yao ya demokrasia na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria.

Guterres alisisitiza ahadi ya Umoja wa Mataifa ya kusaidia juhudi za kitaifa za kuwa na utawala wa kidemokrasia, muungano wa kijamii na kutimiza malengo ya maendeleo endelevu nchini Burkina Faso.

Rais aliyeko madarakani, Roch Marc Christina Kabore alishiriki uchaguzi huo, akisaka muhula wa pili wa miaka mitano, huku akikabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa Eddie Komboigo.

Komboigo ni kiongozi wa chama cha upinzani cha Congress for Democracy and Progress (CDP) chama kilichokuwa cha rais wa zamani wa nchi hiyo, Blaise Compaore.

Compaore alitolewa madarakani na machafuko mashuhuri yaliyozuka nchini humo, mwaka 2014. **RFI**

# Ethiopia yaikatalia AU, Tigray

**Addis Ababa,** Ethiopia

**Wapiganaji wa Tigray, wameahidi kupambana vikali na maadui zao.**


SERIKALI ya Ethiopia imekataa juhudi za Umoja wa Afrika (AU), za upatanisho na kusema wanajeshi wake wamechukua udhibiti wa mji mwingine, wakati jeshi la serikali linapoelekea katika mji mkuu wa mkoa wa kaskazini wa Tigray, unaoshikiliwa na waasi.

Mwishoni mwa wiki, AU uliwateua marais wa zamani wa Msumbiji, Joaquim Chissano, Ellen Johnsof Sirleaf wa Liberia na Kgalema Motlanthe wa Afrika Kusini, kama wajumbe maalum katika mazungumzo ya upatanisho.

Zaidi ya wiki mbili baada ya Waziri Mkuu, Abiy Ahmed kutangaza operesheni ya kijeshi, serikali ilisema vikosi vya usalama vya Tigray, vinaharibu barabara na madaraja, ili kuudhibiti mji mkuu wa mkoa wa Tigray, Mekelle, wenye idadi ya kiasi ya watu nusu milioni.

Wapiganaji wa Tigray, wameahidi kupambana vikali na maadui zao.

Hata hivyo, wamekanusha madai kuwa wameharibu madaraja na barabara. Mamia ya watu wamefariki dunia na wengine 30,000 wakikimbilia nchi ya Sudan, tangu mzozo huo ulipoanza Novemba 4, mwaka huu. **DW**



Ajali ya gari iliyoua wafungwa watano na kujeruhi mmoja, baada ya gari hiyo, kugonga mti. Wafungwa hao walikuwa wakitoroka gerezani mwishoni mwa wiki, Beirut, Lebanon. **PICHA: REUTERS**

## Wafungwa watano Lebanon wafa ajalini

**BEIRUT,** Lebanon

WAFUNGWA watano waliokuwa wakitoroka gerezani, walikufa mwishoni mwa wiki, baada ya gari yao kugonga mti.

Inakadiriwa wafungwa 60 walivunja kituo cha mahabusu cha Lebanon nje ya mji mkuu Beirut, Kikosi cha Usalama cha Ndani cha Lebanon (ISF), kilisema katika taarifa yake.

ISF, haikusema ni jinsi gani wafungwa hao walitoroka kutoka katika kituo hicho, ambacho chanzo cha usalama kilisema kinashikilia wafungwa wa kesi mbalimbali sehemu ya gereza la wilaya ya Baabda, karibu na Beirut.

Rais Michel Aoun, aliarifiwa na waziri wa muda wa mambo ya ndani, juu ya tukio hilo na kwamba shughuli za utafutaji wafungwa hao ziongezwe na tukio hilo lichunguzwe, Ofisi ya Rais ilisema katika ukurasa wake wa tweeter.

ISF, ilisema wafungwa 15 walikamatwa wakati huku watano wakufariki na mmoja kujeruhiwa na kupelekwa hospitalini.

Mnamo Aprili, Amnesty International ilisema kulikuwa na ghasia ndani ya jela za Lebanon na familia zilipanga maandamano, kutaka kutolewa kwa wafungwa wakitilia shaka kuenea kwa COVID-19 katika magereza yaliyojaa watu.

Ilisema serikali ya Lebanon ilichukua hatua kadhaa, pamoja na kutolewa, viongozi wanapaswa kutoa kipaumbele kwa kuwaachilia wafungwa ambao walitumikia vifungo vyao na kuharakisha kesi.

**REUTERS**

## Meli ya mafuta ya magendo mbaroni



**TEHRAN,** Iran

JESHI la Walinzi wa Iran, limeendesha operesheni ya kukamata meli ya mafuta ya magendo na kukamata meli yenye bendera ya Panama, iliyokuwa imebeba lita 300,000 za mafuta ya magendo katika Ghuba ya Uajemi na kuzuia watu 10 waliokuwamo.

Kulingana na taarifa iliyotolewa na kituo rasmi cha habari cha Fars, iliarifiwa kuwa operesheni iliendeshwa na Jeshi la Walinzi wa Mapinduzi dhidi ya meli ya kigeni ambayo iligundulika kubeba mafuta ya magendo kutoka wilaya ya Parsiyan ya Mkoa wa Hürmüzgan.

Katika operesheni hiyo, meli yenye bendera ya Panama, ilikamatwa na wafanyikazi 10 waliokuwamo ndani wakazuiwa.

Taarifa zaidi zilibainisha kukamatwa kwa zaidi ya lita elfu 300,000 za mafuta ya magendo kwenye meli hiyo na hakuna maelezo zaidi yaliyotolewa kuhusiana na uraia wa wafanyakazi waliozuiwa. **TRT**



# ISCO SASA APANGA KUONDOKA MADRID

**MADRID,** Hispania

NYOTA wa Real Madrid, Isco ameripotiwa kwamba anahitaji kuondoka ndani ya timu hiyo inayoshiriki La Liga.

Akiwa chini ya Kocha Mkuu, Zinedine Zidane, ameanza kwenye mechi tatu za LaLiga, huku akishindwa kuanza hata dakika moja kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa Ulaya jambo linalomkosesha raha.

Kwa mujibu wa Marca, Isco raia wa Hispania, akili zake kwa sasa amezielekeza kwenye kutimkia ndani ya kikosi hicho ifikapo Januari ili akapate changamoto mpya kwa kuwa anaona kwamba yeye si chaguo la Zidane.

Zidane amesema kuwa anatambua kwamba Isco anahitaji muda na hawezi kusimama kwenye njia yake ya kutaka kuondoka Januari kwa kuwa ni maamuzi yake yeye mwenyewe.

Ripoti zinaeleza kwamba timu ambazo zinahusishwa kutaka saini yake ni Everton ambayo imekuwa ikihitaji kumsajili kiungo huyo mwenye miaka 28 ambapo sasa anaweza kukutana na kocha wake wa zamani, Carlo Anceotti.

# Solskjaer apagawa ushindi wa kwanza

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amemsifia mwamuzi, David Coote kwa "kufanya maamuzi matatu sahihi" wakati Manchester United ikiibuka na ushindi dhidi ya West Brom.

Penalti ya Bruno Fernandes ya dakika ya 56 pale Old Trafford iliiwezesha Man United kupata pointi tatu, ukiwa ni ushindi wa kwanza nyumbani kwenye Ligi Kuu ya England tangu Julai.

Na Solskjaer alikuwa na furaha kwa ushindi huo wa nyumbani msimu huu akisifia maamuzi ya Coote.

"Tunafurahia kwamba tumepata pointi tatu, ushindi wa kwanza nyumbani msimu huu, tunafurahia na hilo," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

United ipo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikipitwa pointi saba na vinara Tottenham, ambao wamecheza mchezo mmoja zaidi.

Tangu kuanza kwa msimu uliopita, asilimia 16 ya mabao ya Man United kwenye Ligi Kuu yametokana na penalti.





# *Man City kuwafunga tena Sterling, Jesus*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City inapanga kuwaongezea mikataba, Raheem Sterling na Gabriel Jesus kwa mujibu wa gazeti la Mirror.

Kocha Pep Guardiola alisaini mkataba wa kuongeza miaka miwili pale Man City wiki hii, na kumfanya abakie pale kwa miamba hao wa Ligi Kuu England hadi mwaka 2023.

Na sasa Man City inaona kwamba, Sterling na Jesus wanahitaji kupewa mikataba mipya.

Sterling mwenye umri wa miaka 25, mkataba wake wa sasa na Man City unamalizika mwaka 2023, lakini wana matumaini makubwa kwamba atakubali ofa hiyo.

Pia Jesus mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2023, hivyo naye anaonekana kuwa muhimu kwa kikosi hicho.

# Fabregas atoa siri yake na Guardiola

**MONACO,** Ufaransa

CESC Fabregas bado anamchukulia kocha wa zamani wa Chelsea, Jose Mourinho "ni rafiki", lakini amebainisha hazungumzi na Pep Guardiola licha ya kumchukulia kama mtu aliyemvutia zaidi wakati anakua kisoka.

Fabregas kwa sasa akiwa na umri wa miaka 33, anacheza kule Monaco na amekuwa mmoja wa viungo wanotambulika zaidi duniani baada ya kujitambulisha yeye mwenyewe katika kikosi cha kwanza cha Arsenal akiwa na umri wa miaka 16, mwaka 2003.

Tangu hapo amekuwa na kiwango cha kuvutia kabla ya kurudi tena Barcelona – ambako ndiko alikole na kukulia hapo akiwa chini ya Gu diola, akishinda mataji sita kwa mi mitatu.

"Mourinho alikuwa mmoja wa watu walionivutia sana mimi na nikaondoka Barca," alisema Fabregas akiiambia Tot Costa.

"Aliniambia kwamba alikuwa ananifuatilia sana wakati akiwa Chelsea na mimi nikiwa Arsenal, na baadaye tukawa tunafanya wote mazoezi pale Real Madrid wakati nikiwa Barcelona."

Lakini Fabregas amesema licha ya Guardiola kuwa ndiye mtu alitemvutia zaidi yeye, walipofanya kazi pamoja hawakuwa na mahusiano mazuri.

"Sijazungumza na Guardiola muda mrefu sana," alisema.





# HAALAND HASHIKIKI DORTMUND, ULAYA

**DORTMUN,** Ujerumani

ERLING Haaland amemshinda mchezaji mwenzake ndani ya Klabu ya Borusia Dortmund, Jadon Sancho kwenye tuzo ya 'Golden Boy'.

Tuzo hiyo ya Golden Boy ilianzishwa na gazeti la nchini Italia la Tuttosport na imekuwa ikitolewa kwa wachezaji vijana chini ya miaka 21 ambao wamekuwa wakiipambania tuzo hiyo.

Haaland alifunga jumla ya mabao 44 kwenye mashindano yake yote aliyoshiriki kwa msimu wa 2019/20 alipokuwa ndani ya Klabu ya RB Salzburg ambapo alicheza jumla ya mechi 28 kabla ya kuibukia ndani ya Klabu ya Dortmund.

Nyota mwingine ambaye alikuwa anashindana naye ni kutoka ndani ya Klabu ya Atletico Madrid, Joao Felix ambaye alikuwa mshindi wa tuzo hiyo msimu wa 2019.

Haaland amemshinda mchezaji mwenzake wa Dortmund, Sancho, ambaye ni mshambuliaji pamoja na nyota kutoka Barcelona, Ansu Fati na mshambuliaji wa Manchester United, Mason Greenwood.

Pia nyota wa Bayern Munich, Alphonso Davies na yule wa Manchester City Phil Foden walikuwa kwenye mchakato wa kuwania tuzo hiyo.

Matthijs de Ligth alitwaa tuzo hiyo mwaka 2018 na Kylian Mbappe alitwaa msimu wa 2017.

Wayne Rooney, Paul Pogba na Lionel Messi nao pia waliwahi kushinda tuzo hiyo.

Haaland alitupia mabao 11 kwenye mechi 11 alizocheza kwa msimu huu kwenye mashindano yote.

# *Pique aipa pigo Barcelona*

**BARCELONA,** Hispania

MLINZI wa Barcelona, Gerard Pique ameumia goti kwenye mchezo wa kipigo wa Ligi Kuu Hispania dhidi ya Atletico Madrid juzi, Jumamosi.

Mshambuliaji wa Atletico, Angel Correa alimkanyanga Pique na beki huyo kujikuta akishindwa kuendelea na mchezo.


Pique alitolewa nje ya uwanja na bado haijajulikana akataa nje ya dimba kwa muda gani, huku kocha akiachwa kwenye wakati mgumu.

Taarifa za awali zinaonyesha kwamba, Pigue anaweza kuwa nje ya dimba kwa wiki kadhaa na hivyo kuiacha Barcelona katika nafasi ngumu.

Barcelona haijawa na matokeo mazuri tangu kuanza kwa Ligi Kuu Hispania msimu huu na kuumia kwa Pique inaonekana kuwa pigo kubwa zaidi kwao kwa sasa.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MOURINHO AITOA SPURS MBIO ZA UBINGWA EPL

Ni kawaida timu ikishinda inafikiria ubingwa, lakini kwa upande wetu kwa sasa hapana...

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amesisitiza Tottenham haiwezi kutarajiwa kutoa ushindani kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England licha ya kuwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

**Spurs ilionyesha kiwango cha kuvutia wakati ikiifumua Manchester City mabao 2-0 Jumamosi, shukrani kwa mabao ya Son Heung-min na Giovani Lo Celso aliyetokea benchi.**

Kikosi hicho cha Mourinho kimeshinda mechi nne mfululizo, na kina mechi saba ambazo hakijafungwa, lakini kocha huyo raia wa Ureno, ambaye Ijumaa alifikisha mwaka mmoja wa kukaa hapo kwa miamba hiyo ya London, haamini kama kikosi chake kinaweza kupigania taji la Ligi Kuu.

"Najisikia vizuri, pengine kesho (jana) tunaweza kuwa nafasi ya pili tena na hilo si tatizo kwangu, nina furaha tu jinsi mambo yanavyokwenda," alisema akiiambia BBC Sport.

"Watu hawawezi kututarajia sisi kuwa hapa na baada ya msimu mmoja tumepambana na kuwa hapa.

"Hatupigani kwa ajili ya taji, tunachopambana ni kushinda kila mchezo. Lakini tutapoteza mechi na kutoka sare.

"Ni kawaida kuona kwamba timu ikishinda inafikiria ubingwa, lakini kwa upande wetu kwa sasa hapana, bado tuna kazi ya kufanya.

"Kila timu ikiwa uwanjani inawania ushindi na hilo ndilo lengo letu, suala la ubingwa kwa sasa bado sijafikiria."

Mchezaji Son raia wa Korea Kusini amefikisha mabao tisa kwenye Ligi Kuu England msimu huu na kuonekana kuwa kwenye wakati bora zaidi.

## ZISIKUPITE

### CITY KUMFUNGA STERLING

KLABU ya Manchester City iko tayari kutoa ofa ya mkataba mpya kwa mshambuliaji wa kimataifa wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 25. ***(Sunday Mirror)***

### UPAMECANO JINO NJE UTD

MLINZI wa Ufaransa wa timu ya RB Leipzig, Dayot Upamecano mwenye umri wa miaka 22, amependa ujumbe uliotumwa kwa mtandao wa Instagram unaomuhusisha na kuhamia Manchester United. ***(Manchester Evening News)***

### RONALDO KUREJEA MADRID

NYOTA wa Juventus na Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 35, anafuatilia kwa karibu kurejea Real Madrid. ***(Marca)***

### AMFIKIRISHA GUARDIOLA

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amelipa kipaumbele suala la mrithi wa mshambuliaji wa Argentina, Sergio Aguero mwenye umri wa miaka 32 na mshambuliaji wa Benfica raia wa Uruguay Darwin Nunez (21), yuko kwenye orodha hiyo. ***(Sunday Telegraph)***

### JESUS KUONGEZEWA MSHIKO

KLABU ya Manchester City ina uhakika wa kutoa ofa kwa mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 23 na kuongeza kima chake cha mshahara hadi pauni 150,000 kwa wiki. ***(Star on Sunday)***

### GIROUD ATAKIWA MAREKANI

MSHAMBULIAJI wa Chelsea raia wa Ufaransa, Olivier Giroud, 34, amejitokeza kuwa mlengwa wa David Beckham kwa timu ya Inter Miami wakati wa dirisha la usajili litakapofunguliwa Januari mwakani. ***(Sunday Mirror)***

### WIJNALDUM AWANIWA INTER

KLABU ya Inter Milan inamfuatilia kwa karibu nyota wa Liverpool, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30. ***(Corriere dello Sport)***

### ISCO KUONDOKA MADRID

KIUNGO wa Hispania, Isco ameifahamisha Real Madrid nia yake ya kutaka kuondoka huku Madrid ikiwa tayari kumuuza kwa karibu pauni milioni 45, Arsenal na Manchester City zinasemekana kumwinda mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Marca)***

### ROMERO KUUZWA BEI POA

KLABU ya Manchester United iko tayari kumuuza mlinda lango wa Argentina, Sergio Romero, 33, ifikapo Januari kwa kima cha chini cha pauni milioni 2.5. ***(Star on Sunday)***

### ERIKSEN, FRED KUBADILISHANA

KLABU ya Inter Milan itafurahia makubaliano ya mabadilishano na kiungo wa kati wa Denmark, Christian Eriksen, 28 na kiungo wa kati wa Manchester United raia wa Brazil, Fred mwenye miaka 27. ***(Football Italia)***

### CONTE AMCHANA ERIKSEN

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte, amesema kuwa Eriksen ameshapewa fursa nyingi tu za kujiimarisha mwenyewe, lakini bado hajaweza kujiweka sawa. ***(Goal)***

HABARI MICHEZO

## Lusajo aweka rekodi kuibanjua Azam FC

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa KMC FC, Reliants Lusajo ameendelea kuweka rekodi yake na kuwa mwiba mkali mbele ya Azam FC kwa kuwafunga kwa misimu miwili, mfululizo katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Msimu uliopita nyota huyo aliyekuwa katika kikosi cha Namungo FC, alifanikiwa kuwafunga wakati wakishinda kwa bao 1-0 dhidi ya Azam, bao pekee la timu hiyo lilifungwa na Lusajao dakika ya 60, kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi.

Lusajo akiwa katika timu yake mpya kwa msimu huu, amefanikiwa kuendelea rekodi hiyo ya kuwatungua Azam, huku KMC wakipata ushindi wa 1-0, bao pekee akilifunga dakika ya 59, kwenye mchezo uliopigwa Uwanja wa Uhuru jijini juzi.

Mshambuliaji huyo ameliambia gazeti hilo kwamba kabla ya mechi kocha wake, Habib Kondo, alimpa majukumu ya kuhakikisha anakuwa makini na nafasi anazopata ili kupata pointi muhimu katika mchezo huo dhidi ya Azam.

"Ni kweli nimekuwa na bahati ya kuwafunga Azam, nimetimiza majukumu yangu ya uwanjani, kuhakikisha tunapambana kutafuta pointi muhimu katika kila mechi," alisema Lusajo.

## Kocha Mbeya City aona mwanga

**Na Saada Akida**

KAIMU Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Wandiba, amesema ana imani na timu hiyo kufanya vizuri katika mechi zao zijazo kulingana na mabadiliko ya kikosi chake tofauti na awali walivyoanza Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Wandiba alisema kila mechi ameona mabadiliko katika kikosi chake na kumpa matumaini ya kufanya vizuri katika mechi zao zijazo na kuendelea kubaki katika mikikimikiki ya ligi hiyo.

"Nimeona mabadiliko katika kikosi changu, ukiangalia kinavyocheza sasa hivi ni tofauti na awali, nina imani kutakuwa na mabadiliko kila tunapozidi kujiandaa na kupata matokeo mazuri katika mechi zetu zijazo," alisema Wandiba.

Alisema kuna tofauti kubwa ya mechi za awali walizocheza na sasa kwani timu yao imekuwa inacheza vizuri, ila kuna makosa madogo madogo ya washambuliaji na mabeki ambayo yanafanyiwa kazi.

"Ukiangalia katika mechi yetu dhidi ya Ruvu Shooting, umakini wa mabeki na washambuliaji wangu ndio umesababisha kupoteza, naendelea kufanyia kazi upungufu huo ili usijirudie katika mechi zetu zijazo," alisema Wandiba.

# MAMA SAMIA ATOA NENO MCHUANO NBC MARATHON

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI wakimbiaji kutoka Tanzania, Kenya na Uganda wakichuana vikali kwenye mbio za NBC Marathon, zilizofanyika jijini Dodoma jana, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akiwapongeza waandaaji wa mbio hizo, Shirikisho la Riadha Taifa (RT) na Benki ya NBC kwa kuunga mkono harakati dhidi ya saratani ya uzazi.

**Mbio hizo zilizofanyika kwa mara ya kwanza jijini humo, zilivutia washiriki zaidi ya 3,000 kutoka ndani na nje ya nchi ambao walishinda zawadi mbalimbali ikiwamo fedha taslimu na medali kutoka kwa waandaaji.**

Katika mbio hizo ilishuhudiwa Mganda Philip Kiplimo akiibuka mshindi wa kwanza mbio za Km 42.2 kwa kutumia muda wa saa 2:17:26 na hivyo kujishindia Sh. milioni 3.5 wakati Hamis Misai wa Tanzania na Stanley Kipchirchir wa Kenya wakiibuka washindi wa pili na watatu kwa kutumia muda wa saa 2:17:35 na 2: 19:13, kwa mfuatano.

Kwa upande wa wanawake mbio za Km 42, Mkenya Nyawira Muriuki aliibuka mshindi wa kwanza baada ya kutumia muda wa saa 2:40:14 wakati mwenzake, Cheruto Isgah na Mtanzania Natalia Elisante waliibuka washindi wa pili na watatu kwa kutumia muda masaa 2:41:02 na 2:49:26, kwa mfuatano.

Katika mbio za Km 21.1, kwa upande wa wanaume ilishuhudiwa Watanzania wakitamba zaidi kwa kushinda nafasi zote tatu za juu ambapo mwanariadha Gabriel Geay alishinda nafasi ya kwanza kwa kutumia muda wa saa 1:04:28, Fabiano Sule akishika nafasi ya pili kwa kutumia muda wa saa 1:04:49 na Mathayo Sombi akitumia saa 1:04:59 na hivyo kuwa mshindi wa tatu.

Mwanariadha Doreen Chemutai wa Uganda alishinda mbio hizo kwa wanawake ambapo alitumia muda wa saa 1:13:45. Akizungumza kwenye hafla ya kukabidhi zawadi kwa washindi wa mbio hizo, Makamu wa Rais, Samia, aliipongeza Benki ya NBC kwa kushirikiana na RT kuandaa mbio hizo ikiwa ni mkakati wa wadau hao kukuza vipaji vya mchezo huo sambamba kupambana na saratani ya mlango wa kizazi kwa kina mama.

"Shirikisho la Riadha, Benki ya NBC kwa kushirikiana na wadau wengine mmefanya kazi nzuri na huu ni mfano wa kuigwa kwa taasisi nyingine. Saratani ya kizazi imekuwa ikiathiri sana wanawake wengi hapa nchini, hivyo jitihada hizi ni za kuigwa," alipongeza.

Alisema iwapo mchezo wa riadha utatumika vizuri unaweza kuwa na mchango mkubwa katika kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii sambamba na kutumika katika kuongeza uelewa pamoja na kutangaza agenda muhimu za kitaifa ikiwamo utalii.

Aidha, alipendekeza mbio hizo zifahamike kwa jina la NBC Dodoma Marathon huku akiitaka benki hiyo kuiendeleza kwa viwango vya kimataifa zaidi, na kuvutia washiriki wengi wa kimataifa ili ziweze kutumika pia katika kutangaza utalii wa ndani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alikabidhi hundi yenye thamani ya Sh. milioni 100 kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Dk. Julius Mwaiselage, ambaye alibainisha kuwa fedha hizo zitasaidia mapambano dhidi ya saratani katika vituo mbalimbali vya saratani ya uzazi nchini.

Sabi alisema kuwa NBC imeamua kushirikiana na RT kwa malengo mawili ya kukuza riadha nchini na pia kulinda afya ya wanawake kwa kusaidia vituo vinavyohusika na saratani ya shingo ya kizazi, ambayo matibabu yake yanagharimu pesa nyingi.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, pia alisema serikali imejipanga kusaidia sekta ya michezo nchini kwa kutenga fungu maalum kwa ajili ya kusaidia vyama vya michezo.

Rais wa Shirikisho la Riadha Taifa, Anthony Mtaka, ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, yeye aliishukuru Benki ya NBC kwa ushirikiano na uwekezaji mkubwa katika mchezo huo, uamuzi ambao awali uligonga mwamba kupitia taasisi nyingine za kifedha.

Alisema kupitia ushirikiano huo unaohusisha ufadhili, fedha kiasi cha Sh. milioni 300 kutoka benki ya NBC ni wazi utainua mchezo huo nchini pamoja na kuzifanya mbio hizo kuwa miongoni mwa mbio kubwa katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati zikifanyika jijini Dodoma kwa miaka mitano mfululizo.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi, akimtunuku medali mmoja wa washindi wa mashindano ya NBC Dodoma Marathon, jijini Dodoma jana, ambapo mgeni rasmi alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan. **MPIGAPICHA WETU**

# *Mgunda alia na wachezaji kupigwa wiki*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, amesema kufungwa mabao 7-0 dhidi ya Simba kumetokana na uzembe wa wachezaji wake kufanya makosa yanayojirudia.

Akizungumza kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha baada ya mechi hiyo ya juzi, Mgunda alisema mabao yote ambayo Simba wameyapata kwenye mchezo huo, yanatokana na wachezaji wake kufanya makosa yanayojirudia na wenzao wakawa wepesi wa kuyatumia na kuyageuza kuwa magoli.

"Nakubali matokeo, tumefanya uzembe wenyewe. Tumefungwa mabao mepesi kwa uzembe wetu wenyewe. Kuna watu wananiambia kuwa nisingefunguka, tatizo siyo kufunguka wala kufunga, magoli tuliyofungwa si kwamba tulizidiwa sana, tunafanya makosa ya kujirudia na kwa kiwango cha wachezaji kama wa Simba ni lazima wakuadhibu," alisema.

Mgunda, straika wa zamani wa timu hiyo, alisema kuwa angalau kipindi cha pili, wachezaji wake walijirekebisha na hii ni baada ya maelekezo ya kipindi cha pili.

"Tulichojifunza ni kwamba tukifanya makosa tutaadhibiwa. Na kwa hili lililotokea hata tukianza kujadiliana hadi kesho hatutapata muafaka, mechi imeisha na cha kufanya ni kuangalia mechi inayofuata," alisema.

Baada ya kipigo hicho, Coastal inakamata nafasi ya 13, ikiwa na pointi 12 kwa mechi 11 ambazo imecheza wakati huu kesho ikiikaribisha Ihefu kwenye uwanja huo huo wa Sheikh Amri Abeid.

# Michezo

Jumatatu Novemba 23, 2020

Nipashe




Mourinho aitoa Spurs mbio za ubingwa EPL UKURASA 22

MARATHON...



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan (katikati), akishiriki mbio za NBC Dodoma Marathon 2020, zilizofanyika jijini Dodoma jana na kushirikisha wanariadha 3,000 kutoka Tanzania, Kenya, Malawi na Uganda. **HABARI UK. 23**

## Azam yakiri KMC maji ya shingo

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amefichua siri ya kupoteza mbele ya KMC FC kwanza akikiri kuwa wapinzani wao walikuwa bora zaidi mwanzo mwisho wa mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, iliyomalizika kwa kukubali kipigo cha bao 1-0 katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Vivier alisema timu yao ilipambana kutafuta pointi tatu, lakini KMC walifanikiwa kuziba njia zao zote na kucheza katika ubora wa hali ya juu katika dakika zote 90 na kustahili kupata udhindi huo.

Alisema wanakubali kikosi chao juzi hakikucheza katika ubora wao kama ambavyo wamekuwa wakionyesha kwenye michezo iliyopita, na kwamba hiyo ni hali ya kawaida na kwenye mpira wa miguu hutokea timu kutokuwa vizuri kila siku.

"Kwa sisi hatukuwa vizuri kwenye mchezo dhidi ya KMC, mambo kama hayo hutokea hata kwenye maisha ya binadamu ya kila siku huwezi kuwa sawa, pia kutokuwa na baadhi ya wachezaji wakiwamo Nicholas Wadada, Frank Domayo na Salum Abubakari hiyo haiwezi kuwa sababu ya kupoteza mechi hiyo."

# Sven awaonya Simba wakiivaa Plateau

**Na Mwandishi Wetu**

### ●●● Ni wakati Wanaigeria hao wakizuga kuwa hawajawa tayari, watanguliza mashushu huku akiwataka...

LICHA ya ushindi wa mabao 7-0, walioupata dhidi ya Coastal Union ya Tanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amewaonya wachezaji wake kutobweteka na matokeo hayo kuelekea mchezo wa mtoano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Plateau United ya Nigeria.

**Simba ambayo katika mechi hiyo ya juzi haikuwatumia baadhi ya mastaa wake akiwamo, Luis Miquisson, Chris Mugalu, Meddie Kagere, Jonas Mkude na Rally Bwalya, inatarajiwa kuifuata Plateau United Jumatano tayari kwa kushuka dimbani nchini humo Ijumaa wiki hii kabla ya timu hizo kurudiana Desemba 4, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.**

Tayari Sven alishaeleza malengo yake kuwa ni kupata matokeo katika mechi zote mbili ya ugenini na nyumbani dhidi ya wapinzani wao hao ambao ndiyo kwanza wapo kwenye maandalizi ya msimu mpya kutokana na ligi nchini mwao kuchelewa kuanza kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya corona.

Lakini kutokana na matokeo ya juzi, shukrani zikiwaendea mshambuliaji na nahodha wa timu hiyo, John Bocco aliyepiga hat-trick, kiungo Clatous Chama aliyetupia mawili, Hassan Dilunga 'HD' na Bernard Morrison kila mmoja akicheka na nyavu mara moja, Sven alisema juhudi na akili zao sasa wanapaswa kuzielekeza dhidi ya Plateau na kutobweteka na ushindi huo.

Sven alisema, mchezo huo wa Ligi ya Mabingwa ni tofauti kabisa na huo wa Ligi Kuu na kila mchezaji anapaswa kujituma vilivyo ili waweze kutimiza malengo yao ya kufika hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.

"Malengo yetu ni kushinda, lakini hautakuwa mchezo mwepesi na wachezaji wanapaswa kutobeba matokeo haya," alisema Sven.

Kwa upande wa nahodha wa Simba, Bocco alisema sasa wanageukia mechi hiyo dhidi ya Plateau na wanafahamu utakuwa mchezo mgumu tofauti na mechi za Ligi Kuu, lakini wao kama wachezaji watapambana kuhakikisha wanapata matokeo.

"Kwanza niishukuru kwa kumaliza mechi hii salama na kushinda, kuhusu mechi ya Ligi ya Mabingwa natambua haitakuwa rahisi, lakini tunakwenda kupambana," alisema Bocco.

Katika hatua nyingine, taarifa zilizolifikia Nipashe jana kutoka chanzo chetu ndani ya Simba, zilieleza kuwa tayari klabu hiyo imetuma mashushu wake kwenda kuweka mambo sawa Nigeria kabla ya timu kuwasili nchini humo.

"Unajua Simba si klabu ngeni katika mashindano haya, hivyo haiwezi kwenda kichwa kichwa, tayari Abasi [Ally], ametangulia kuweka mambo sawa," Nipashe lilipenyezewa.

Hata hivyo, si Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba (CEO), Barbara Gonzalez wala Msemaji wao, Haji Manara aliyekuwa tayari kupokea simu Nipashe lilipowatafuta jana ili kuthibitisha taarifa hiyo na kuzungumzia safari ya timu hiyo kwa ujumla.

Kwa upande wa wapinzani wao, ambao wamekuwa wagumu kuzungumzia mchezo huo mara kwa mara kupitia vyombo vya habari, Ijumaa iliyopita, Kocha Mkuu wa Plateau United, Abdu Maikaba, alisema kikosi chake kitakuwa tayari kwa muda muafaka kuelekea mechi hiyo ya CAF dhidi ya Simba.

Makaiba ambaye kwa sasa na kikosi chake cha Plateau wamejichimbia mjini Aba, Kusini Mashariki mwa Nigeria, kwa ajili ya michuano midogo ya maandalizi ya msimu mpya, aliiambia Brila.net kuwa ingawa timu yake haijawa kamili vyakutosha kuelekea mechi hiyo ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa, wanapaswa kujiandaa kwa wakati kuwa fiti kwa mchezo huo.

"Hatujajiandaa vyakutosha kwa ajili ya mechi hii ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini ninaamini kwa siku 10 zijazo (kuanzia Ijumaa iliyopita), tutakuwa kamili maeneo yote kwa mbinu za kutekeleza katika mechi hiyo.

"Nimewaambia vijana wangu kuwa baada ya mashindano haya (ya kujiandaa na msimu mpya), lazima tuwe tayari kwa ajili ya kuivaa Klabu ya Simba kwa sababu hatuna muda mwingi. Inaonekana kiwango chetu cha mazoezi kimwili kina alama ya maswali na natumai mchezo wa kesho (Jumamosi) utakuwa bora. "


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042